# *Kipeo Cha Mungu Kilichotambulishwa*

Asante, sana, ndugu. Billy anataka niseme ya kwamba hii ndiyo mara yangu ya kwanza mimbarani, kwa muda wa miezi mitatu. Naye . . . Nakumbuka mara ya kwanza nilipomleta, hapa kushuhudia, alisema, "Jambo la kwanza, ninaogopa." Mimi, pia. Karibu miaka thelathini na mitano katika huduma, na huu ndio wakati mrefu sana sijapanda mimbarani tangu nilipoingia katika huduma. Nilihitaji kupumzika kidogo, kwa hiyo mimi na Ndugu Mosley, na baadhi ya ndugu hapa, tumekuwa katika safari ya muda mfupi ya kuwinda. Na sasa tumekwisha kupumzika. Na huu ndio mkutano wangu wa kwanza tangu ni ninii . . . mnamo tarehe moja Septemba. Na ni jambo muhimu. Huduma ni jambo ambalo kwa namna fulani unapaswa kuendelea nalo?

2 Na sasa nimewaomba wazime hicho kiyoyozi, ama waone kama wangeweza kukizima, kwa maana ninajua ni vigumu kusikia. Na ni vigumu, najua wakati mtu fulani anatoa ushuhuda wao. Ilikuwa vigumu kwangu kuwasikia. Je! mnaweza kusikia vizuri sasa? Vyema. Ninajua kusimama kwa namna fulani karibu na maikrofoni hii mpaka watakapotengeneza hiyo.

3 Haya bila shaka ni majaliwa ma—makubwa kwangu, na bila shaka ni—ninamshukuru mwenyekiti, na kwa tawi la Wafanyibiashara wa Full Gospel hapa Yuma, na kwa wahudumu wote. Waimbaji hawa wazuri hapa, waliokuwa hapa muda mfupi uliopita, ningetaka kuwasikia m—mkutanoni. Huo ulikuwa ni uimbaji mzuri kweli. Ni—nilishangaa sana, wakati walipokuwa wakiimba, kama Yohana aliniona. Nami natumaini ya kwamba aliniona. Na, kwa hiyo, ninasikia mko katika ufufuo hapa. Bwana awabariki sana, ndugu na dada, mnapohudumu. Na marafiki wangu wote huko Phoenix na sehemu mbalimbali, ambao . . . na kutoka kote California.

4 Nami ninataka kusema neno moja juu ya matawi haya. Nilipokuja kwa watu wa Kipentekoste, nilikuwa . . . nilikuwa nimepata ujuzi wa kipentekoste, bila kujua ya kwamba kulikuwako na kanisa la Kipentekoste. Nilikuwa Mbaptisti wa Kimishenari wakati huo. Nilipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, nami nikakuta kwamba kulikuwako na watu ambao waliamini jambo lile lile nililokuwa nimepokea. Nao walikuwa wamelipokea miaka arobaini kabla sijalipokea. Kwa hiyo nilikuwa tu mmoja, kama Paulo alivyosema, ninaamini, si kujaribu kusema pamoja naye, lakini kwa namna fulani "mimi nimezaliwa wakati usiofaa." Lakini ninii . . . Ilionekana ndugu

zangu walidhani nimerukwa na akili, nimeingia kichaa, kama tunavyosema. Lakini ni—nilijua ya kwamba nilkuwa nimepokea kitu fulani. Kwa hiyo, tukio langu lilikuwa kama tu lile walilokuwa nalo kule. Na hivyo ndivyo ninavyotaka jambo hilo.

5 Na, hata hivyo wakati nilipokuja miongoni mwao, ja—jambo la kuvunja moyo kuhusiana na hilo, nilikuta kwamba walikuwa wamegawanyika tu, katika makundi mbalimbali ya kimadhehebu, karibu kama tu kanisa langu la Kibaptisti lilivyokuwa. Nao. . . Nilifikiri kulikuwa na moja tu lililoitwa Pentekoste, na lilikuwa ndilo hilo tu. Bali, nilikuja kugundua, kulikuwa na madhehebu yao mengi. Kwa hiyo, sasa, wote walikuwa walikuwa ni watu wazuri. Ninajua baadhi ya watu wazuri sana niliopata kukutana nao, maishani mwangu, walikuwa katika makundi haya. Nao walikuwa—walikuwa, bila shaka, madhehebu mbalimbali. Na ninii langu—wazo langu lilikuwa ya kwamba tunapaswa kuwa katika moyo mmoja, pamoja na Kristo, wala kamwe sikujiunga na madhehebu yo yote yao fulani. Nilikaa tu katikati yao, na nikijaribu kushika mikono yote miwili, na mikono yote, na kusema, "Sisi ni ndugu." Hatuninii. . . Tunaweza kuona mambo madogo madogo tofauti, mmoja kutofautiana na mwingine. Lakini, mbali na hayo yote, sisi tungali ni ndugu, kwa kuwa tumezaliwa na Roho yule yule. Sisi ni familia ya Mungu.

6 Ndipo wakati wafanyabiashara Wakristo, Wafanyabiashara wa Full Gospel, tawi hili, nilikuwa miongoni mwa mikutano ya kwanza pamoja na Ndugu Shakarian. Nilimjua kabla hapajakuwa na shirika hilo, ama chombo hiki kuanzishwa. Nilikihesabu kuwa ni chombo ki kuu. Na kimekuwa ni mlango uliofunguliwa kwa ajili yangu, kusafiri kote duniani pamoja na Wafanyibiashara wa Full Gospel.

7 Ambapo, mara kwa mara, kwamba unaona kundi la wahudumu, wakati fulani, wanakuwa na hisia ndogo dhidi ya kundi lingine, kwa sababu eti mtu fulani alisema jambo fulani. Hilo si kila mahali, bali tunaliona jambo hilo katika sehemu-sehemu. Na kwa mfano, kama kanisa moja litalidhamini kundi hilo, hilo lingine halitajihusu nalo.

8 Lakini kwa Wafanyabiashara wa Full Gospel, wamekuwa ni mlango uliofunguliwa kwa ajili yangu. Wanapoingia, ndipo ninawakusanya ndugu zangu wote pamoja, nasi tu—tunaweza kushirikiana; pengine wachungaji wawili huenda walikuwa na hisia fulani, ama kitu fulani. Huu umekuwa ni mlango mkubwa uliofunguliwa, nami nimesafiri kote ulimwenguni kwa ajili yao sasa kwa miaka kadhaa, nikihubiri kwenye matawi yao.

9 Na Yuma haina mji mkubwa sana, ingawa ninakisia ni mkubwa zaidi ya ule niliotoka, Jeffersonville, Indiana. Lakini nilikutana na mwenyekiti wenu hapa. Ninii. . . alikuwa. . . na watu mbalimbali wa tawi lenu. Nami nafikiri mna nafasi nzuri sana hapa.

10 Nilikuwa tu nikifikiri, usiku wa leo, wakati nimeketi hapa na kuwaangalia watu. Unajua, hivi karibuni tutanyang'anywa majaliwa haya. Baraza la Makanisa Ulimwenguni hivi karibuni litatumeza. Ninadhani ya kwamba karibu wasikilizaji wangu wote usiku wa leo ni Wapentekoste, na Wabaptisti, na—na Kanisa la Mungu, na hao walio nje ya Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Na—na wao, hayo ndiyo waliyochezea tu, na hivyo ndivyo Biblia ilivyosema wangefanya. Nasi tumeonywa juu ya jambo hilo, kwa hiyo hebu na tusilikaribie. Na kwa hiyo kama ilivyokuwa ikisemwa usiku wa leo, katika ule wimbo, juu ya kukaribia kwa Kuja kwa Bwana, huenda kumekaribia zaidi ya tunavyowazia kumekaribia.

11 Nami nafikiri ni wakati tunapoweza kukutanika katika ushirika wa namna hii, linatufanyia jambo fulani, ambalo linatuvuta karibu zaidi mmoja kwa mwingine. Na tunavyokaribiana sisi kwa sisi, tunamkaribia pia Mungu, kwa maana Yesu alisema, "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa walio wadogo sana wa hawa watoto Wangu, mmenitendea Mimi."

12 Nina mvulana mdogo hapa ndani yuko mahali fulani, nadhani, Joseph. Nina Billy anayeketi hapa. Binti wawili wanaoketi kule nyuma, na mke. Sasa kama mtu ye yote alikuwa na kitu ambacho kilikuwa . . . ulitaka kufanya kitu kilicho kizuri sana, kwangu mimi ni afadhali sana iwapo ungeliwatendea watoto wangu kuliko kunifanyia mimi. Na kwa hiyo ninajisikia labda, mimi kama mzazi . . . Na Yeye ndiye chimbuko cha kuwa mzazi. Nafikiri kwamba hivyo ndivyo Mungu anavyojisikia. Kama tungeninii . . . Tunamtumikia tunapotumikiana mmoja kwa mwingine. Hivyo ndivyo tunavyomtumikia Mungu.

13 Na tukijua jambo hili kuwa ni kweli, basi nafikiri kwamba kila wakati tawi hili linapokutana, kwa kuwa linasimamia makanisa ya kiinjilisti. Hakuna hasa fundisho la kibinafsi ambalo Wafanyibiashara wa Full Gospel wanatetea. Wao wanatetea tu Injili nzima. Na kama mtu fulani akiwa na maoni ya tofauti, hilo ni sawa kabisa. Ni sawa. Tuna ushirika pamoja, hata hivyo. Kwa hiyo ninafikiri ya kwamba lingekuwa ninii . . . Kama ningaliishi hapa katika jiji hili, ninaamini, wakati tawi hilo lilipokutana, kama kungalikuwa na njia yo yote inayowezekana hata kidogo, ningekwenda kule na kumleta kila mtu aliyeko kule ambaye ningaliweza kumleta. Hiyo ni kweli, kwa sababu ni ja-—ni jambo linalotutia nguvu kwa pamoja.

14 Mimi ninaishi huko Tucson, na mimi mara kwa mara ninahubiri kwenye tawi hilo, wakati wote. Na huko Phoenix, tangu nilipohamia Arizona, niko huko Phoenix wakati wote ninapopata nafasi ya kuondoka na kwenda—kwenda Phoenix. Kwa sababu ya ninii, na kujaribu kumleta mtu fulani, kumwalika mtu fulani, kuwaita wahudumu wengine.

Nao husema, “Vema, vema, unaona, Ndugu Branham, hatuninii.”

15 Ninasema, “Haijalishi vile unaninii. . .Hebu twende sote. Twende kama ra—rafiki, pamoja nami.”

16 Na uwafikishe wakae kule kwa muda mfupi. Hivyo ndivyo tu unavyopaswa kufanya. Nao wanaona, kila mtu moyo wake una njaa ya ushirika. Nasi tunapaswa kuwa tukifanya hivyo. Ni ishara kubwa ya wakati wa mwisho. Mungu na alibariki tawi hili. Na lininii—na lidumu mpaka Bwana Yesu atakapokuja kutupokea Utukufuni, ndilo ombi langu.

17 Sasa, ninakumbuka ziara yangu ya kwanza ya kupitia Yuma. Nilikuwa katika Fordi ya Muundo wa T ambayo iliweza kusafiri maili thelathini kwa saa. Nilikuwa nikiwazia nilipokuja nikiendesha gari leo. Ningali niko mwaminifu kwa Ford; ningali nina moja, wala sikuwa na kitu kingine cho chote ila hiyo. Lakini mimi. . .Sasa, siuzi Ford. Sasa, hayo si matangazo yake ya biashara. Unaona? Lakini ninakumbuka jinsi ambavyo hiyo Ford. . .Wengi wenu ndugu mlio na umri kama wangu mnakumbuka ule Muundo wa T wa kale. Hii ilikuwa ni ya mwaka wa 1927. Ilibidi uangalie kwa makini sana la sivyo usingeweza kuuona Yuma ulipopitia hapa. Ulikuwa ni mdogo sana, na kwa kweli mji wenu umepanuka. Lakini, jinsi nilivyopata maili zangu thelathini kwa saa kwenye Ford yangu ni kwamba, ilienda maili kumi na tano *huku*, maili kumi na tano *huku*. Kwa hiyo, zikijumlishwa pamoja, nilikuwa na maili thelathini kwa saa, pamoja na kurushwa-rushwa kote kwangu na kadhalika. Yuma imepanuka.

18 Kanisa hili tukufu, ambalo tuna—tunashindania kwa ajili ya Imani hii ya ajabu.

19 Asante, ndugu, ye yote yule aliyefanya jambo hilo. [Mtu fulani alimpa Ndugu Branham kitu fulani—Mh.]

20 Umepanuka, pia, nasi tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo. Bwana na awabariki ninyi nyote.

21 Tunatumaini, kama upo, karibu, kwenye mikutano yo yote hii. . .Nitalihubiria ta—tawi la Phoenix, Jumapili ijayo. Na Jumapili ifuatayo huko Flagstaff. Na Jumatatu ifuatayo, tarehe ishirini na moja, ni dhifa huko Tucson. Wote mnaalikwa.

22 Na, Bwana akipenda, ninataka kuzungumza kwenye bwalo la dansi la Mote-. . .Hoteli ya Westward Ho, ninaamini. Huo unaanza kwenye usiku upi? [Mtu fulani anasema, “Hilo ni Jumapili alasiri, tarehe ya kumi na saba.”—Mh.] Jumapili alasiri, tarehe kumi na saba, ibada ndogo tu ya kiinjilisti. Natumaini waimbaji hawa watakuwapo, wakati huo ukikaribia, kutusaidia. Nasi tutakuwako huko mpaka Jumatano. Ninafikiri ni Jumapili alasiri. Nasi tunafanya jambo hilo kwa maana hatutaingilia mipango yo yote ya makanisa. Halafu, Jumatatu na Jumanne, halafu Jumatano tuko kule Ra-. . .kwenye West-. . .Hoteli ya

Ramada, Hoteli ya Ramada. Na halafu Alhamisi tutaanzia Westward Ho. Ni sawa?

23 [Ndugu fulani anasema, "Westward Ho, Jumapili, Jumatatu, Jumanne. Ndipo tutaenda kwenye Hoteli ya Ramada, Jumatano, na tutakaa kule mpaka mkutano utakapoisha."—Mh.] Mkutano utakapoisha, kwenye Hoteli ya Ramada. Kwa hiyo tutafurahia kuwa pamoja nanyi wakati wo wote.

24 Sasa, kabla hatujafungua Kitabu hiki, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu na kuzungumza na Mwandishi.

25 Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa kwenye mavumbi ambako Mungu alitutoa, na, Yesu akikawia, hatuna budi kurudi huko siku moja. Tangu tu nilipokuwa hapa, nilipokea ujumbe kutoka mashariki, ya kwamba maskini bibi mmoja niliyemfahamu. . . Ni msichana mdogo aliyeitwa Edith Wright. Ameenda kukutana na Mungu, alasiri ya leo, saa tisa. Inatubidi kurudi. Kama kuna mtu ye yote hapa ambaye angetaka kukumbukwa katika maombi, naomba umwinulie Mungu mkono wako. Mungu akubariki.

26 Baba wa Mbinguni, kama ambavyo tumeufurahia sana ushirika huu mzuri, kuimba, loo, jinsi ulivyoufurahisha moyo wangu nilipousikia ule wimbo, *Je! Yohana Aliniona*? Baba, ninatumaini ya kwamba sote tutakuwako kule, kila mmoja wetu. Nasi tumeinama sasa tumesujudu kuelekea kwenye mavumbi, nasi tu—tunaomba kwamba utapokea kushukuru kwe—kwetu, na toba yetu, na maombi yetu ya mmoja kwa mwingine.

27 Na sasa tunaligeukia Neno Lako, ile sehemu takatifu ya mkutano ambayo inaonekana ni takatifu zaidi kuliko—kuliko nyingine, kwa maana tunajua kwenye wakati huu tunawashughulikia watu, kuwaongoza kwenye Kweli, kwa Kristo na kwa Neno, ambalo ni Kristo. Nasi tunaomba ya kwamba utatufungulia Neno. Tu—tu wapungufu, Bwana, bali Wewe unatosha kabisa. Kwa hiyo ninaomba ya kwamba utabariki jitihada zetu nyonge, na utujalie sisi usiku wa leo tujikute na tujitafutie nafasi yetu katika Neno la Mungu. Tujalie, Baba. Nasi tutakupa sifa, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

28 Sasa, hii ni hali nzuri sana kuwa hapa. Nina mihtasari michache hapa ambayo nilifikiri ningeirejea, kwa dakika chache, kwa kuwa sidhani tunaruhusiwa kuushikilia ukumbi huu kwa muda mrefu sana jioni. Na kwa namna fulani mimi, pia, nikiwa miongoni mwa Wapentekoste, kwa namna fulani mimi huenda polepole, mwajua.

29 Ninakumbuka, nimewaambia, labda. Nilipomwona mhudumu Mpentekoste kwa mara ya kwanza, ilikuwa ni Kasisi Robert Daugherty kutoka St. Louis. Nina shaka kama ye yote wenu alimjua. Mmeona ushuhuda wa msichana wake mdogo

katika kitabu. Alikuwa—alikuwa . . . Aliponywa ugonjwa wa dansi la Mt. Vitus, na alikuwa amekatiwa tamaa. Na hivyo ndivyo nilivyokutana na Wapentekoste wa kwanza.

30 Na, kuhusu jambo hilo, nilienda kumsikia akihubiri, na—na, jamani, a—aliweza kuhubiri. Angeninii . . . Hata asingengojea kitu cho chote. Naye angehubiri mpaka angeishiwa na pumzi, naye angekuwa bluu usoni, na magoti yake yangegongana, na karibu angeanguka sakafuni. Ndipo angerudiwa na na pumzi yake, ungeweza kumsikia huko kwenye vitongoji vya mji, karibu, halafu anasimama akihubiri. Nami nikawazia, "Jamani, ni—nisingeweza kuyawazia upesi namna hiyo."

31 Inanibidi tu kwa namna fulani kuchukua wakati wangu. Kwa namna fulani mimi huenda pole pole, na ninazeeka, pia, ninyi mnajua, nikitambaa, kwa hiyo ninatumaini mtanivumilia kwa dakika chache.

32 Kuna jambo moja la hakika, ninalojua halitashindwa, na hilo ni Neno Lake. "Mbingu na nchi vitapita, bali Neno Lake halitashindwa kamwe." Kwa hiyo hebu na tufungue sasa, kama una Biblia yako, na mngetaka kusoma kutoka kwa Hilo, katika Kitabu cha Isaya, mlango wa 53 wa Isaya. Ningetaka kusoma hili kwa ajili tu ya kujenga, kupata fungu la kujenga juu yake fungu la maneno, kwa muda kidogo.

*Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? Na mkono wa* B*WANA* *amefunuliwa nani?*

*Maana alikua mbele zake kama mche mwororo, na kama mzizi katika nchi kavu; yeye hana umbo wala uzuri; na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani.*

*Alidharauliwa na kukataliwa na watu; mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu.*

*Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, amepigwa na Mungu na kuteswa.*

*Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.*

*Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na* B*WANA* *ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.*

*Alionewa, lakini alinyenyekea, wala hakufunua kinywa chake; kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, na kama vile kondoo anyamazavyo mbele yao wakatao manyoya yake; naam, hakufunua kinywa chake.*

*Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa; na maisha yake ni nani atakayeisimulia? Maana amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu.*

*Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; na pamoja na matajiri katika kufa kwake; ingawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na hila kinywani mwake.*

*Lakini* B*WANA* *aliridhika kumchubua; amemhuzunisha; utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi, ataona uzao wake,* na *ataishi siku nyingi, na mapenzi ya* B*WANA* *yatafanikiwa mkononi mwake;*

*Ataona mazao ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki; naye atayachukua maovu yao.*

*Kwa hiyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu, naye atagawanya nyara pamoja na walio hodari; kwa sababu alimwaga nafsi yake hata kufa, akahesabiwa pamoja na hao wakosao. Walakini alichukua dhambi za wengi, na kuwaombea wakosaji.*

33 Ninataka tu kusema jambo hili, kwa somo dogo tu. Ninataka kuchukua somo kutoka hapo, kama: *Kipeo cha Mungu Kilichotambulishwa.*

34 Sasa, hili lingekuwa so—so—somo kweli kweli la kusoma, kutoa kipeo kwake. Lakini tunapoliangalia, kama ambavyo tungeliwazia, hicho kingekuwa ni kitu kingine cho chote mbali na kipeo, kwa maana lilisema, "Tulimficha nyuso zetu, wala hakuwa na uzuri hata tumtamani." Na mara nyingi, mambo fulani tungeita kipeo, ambapo Mungu asingemaanisha kitu hicho kabisa. Kwa sababu, hekima ya mwanadamu ni upuuzi kwa Mungu, bali upuuzi wa Mungu una hekima zaidi ya hekima zote za mwanadamu.

35 Nasi tunaona hapa, ya kwamba Mungu alitupa picha ya jambo fulani. Ningetaka kujaribu kuleta picha hii mbele yetu, kwani ninatambua kwamba huenda ukawa ndio wakati wa mwisho ambao baadhi yetu akapata tunakutana pamoja. Huenda tusionane tena kama tulivyo sasa. Kwa hiyo, kama tumekusanyika kwa kusudi hili, si kuonwa au kusikiwa . . .

36 Lakini tulikuwa na ushirika wetu wa sisi kwa sisi tulipokuwa tuhudumiana chakula hiki kitamu sana usiku wa leo, mezani, tulipoilisha miili yetu ya kibinadamu, na sasa tungetaka Mungu ailishe nafsi yetu Mana Yake iliyofichwa. Ni kwa wale makuhani tu ambao wameingia katika Patakatifu pa patakatifu wanaoruhusiwa kula Chakula Chake.

37 Na kama tulitambua, usiku wa leo, steki ye-yetu. Siamini nimepata kuwa na dhi—dhifa hata sasa, katika mahali pote nilipofanya mikutano, kama usiku wa leo, ambapo nimepata kula steki nzuri kama waliyotuandalia usiku wa leo. Sasa, unaona, ilitubidi kula hiki kwa sababu kwamba; kama tunaishi, ilibidi kitu fulani kife tupate kufurahia wakati huu wa ushirika, na pia kuyadumisha maisha yetu.

38 Nilikuwa nikizungumza na mtu fulani ambaye ni mla mboga za majani, si muda mrefu uliopita, naye akaniambia, "Vema, si—sikubaliani nawe." Vema, kwa namna fulani ali—alinipa barua, alitaka kukutana nami faraghani. Naye akasema, "Ndugu Branham, daima nilikustahi wewe kama mtu mtakatifu." Akasema, "Bali nilipokusikia ukisema ulikula nyama ya paja la nguruwe na mayai kwa ajili ya kiamshakinywa," kasema, "hilo—hilo lilinivunja moyo."

39 Vema, kuhusu hilo, nisingeweka jiwe la kujikwaa mbele zake. Sasa, hivyo ndivyo anavyoamini. Lakini nilisema, "Vema, bwana, nisipokula, sitaishi."

40 Akasema, "Lakini, unaona, ilibidi ule nguruwe, na—na uchinje kuku."

41 Nikasema, "Bwana, tunaishi tu kwa vitu vilivyokufa. Sijali unakula nini. Ukila mboga. Ukila. Ukila mkate, hiyo ngano ilikufa. Ukila mahindi, mahindi yalikufa. Ukila maharagwe, maharagwe yalikufa."

42 Chochote ulacho, unaweza tu kuishi kwa mwili wa udongo sababu kitu fulani kilikufa ili upate kuishi. Sasa, lolote ufanyalo, hata kunywa maziwa, bakteria, chochote kile, inakubidi kuishi kwa vitu vilivyokufa. Na linaenda tu kuthibitisha, kama itatubidi kuishi maisha haya ya kawaida, nasi tunaweza kufanya hivyo tu kwa vitu vilivyokufa, ilibidi kitu fulani kife ili uweze kuishi Milele. Huyo ni Yesu Kristo, ambaye Mungu alitupa kama fidia.

43 Na sasa, wakati nilipokutana na Wapentekoste kwa mara ya kwanza, ni—nilienda California, mkoa tu unaopakana na huu hapa, upande wa pili wa mto. Nami nilikuwa huko Los Angeles. Sikuishi kamwe katika siku za bibi huyu mhudumu anayejulikana sana, Bibi Semple. . . Aimee Semple McPherson. Nilikutana na mwanawe, Rolf, muungwana mzuri Mkristo, na—na mke wake na familia yake. Kwa kweli wao ni watu wazuri sana, na Dk. Teeford na wengi wa wafanya kazi huko kwenye Hekalu la Angelus. Nami nilihubiri Yubile ya Pentekoste, Yubile ya miaka hamsini kule, miaka michache iliyopita, na kwa kweli nilikuwa na wakati mzuri sana.

44 Kwa hiyo kwa heshima ya mwanamke huyu aliyeweka mfano kama alivyofanya, wa kujaribu yote awezayo, na ku—kutoa kilichokuwa moyoni mwake, nilienda kutoa heshima kwa ajili kwenye kaburini lake huko Forest Lawn. Na nilipokuwa

nimesimama pale huku nimevua kofia yangu, na—na kuinamisha kichwa changu na kumshukuru Mungu kwa ajili ya maisha ya tabia nzuri ya maskini mtumishi mwanamke huyu, niliombwa baadaye na hicho kikosi nilichokuwa pamoja nacho, kundi la wahudumu, kama ningefanya matembezi kwenye. . .kote katika Forest Lawn. Na kuingia ndani ya jumba la maiti pale, ama cho chote unacholiita, nilikuwa nikiangalia usanifu wake mbalimbali, ndipo nikaona Meza ya Bwana, na nikasimama. Wengi wenu mmeiona, wakati walipoiwashia taa ile, Meza ya Bwana, na mmesikia hadithi hiyo yake.

45 Lakini moja ya mambo ya kuvutia macho sana niliyoyaona pale, ilikuwa ni wakati unapoingia mlangoni, ninaamini ingekuwa ni kuelekea upande ule wa mashariki. Kulikuwa na sanamu ya Musa iliyowekwa pale, ambayo ilikuwa ni kifuniko cha kazi ya mikono ya maisha ya Michelangelo, ninaamini ndiye, mfinyanzi. Hapo, huenda nimekosea jina la mtu huyo. Ninaamini hiyo ni kweli. Michelangelo, ambaye—ambaye. . . yule mfinyanzi hodari aliyeifinyanga hii, ama sanamu ya Musa. Na wakati alipokuwa akiielezea, yule—yule kiongozi aliyekuwa akitutembeza, alisema ya kwamba hiyo ilikuwa ni moja ya vipeo maarufu sana ambavyo Michelangelo aliwahi kufinyanga. Naye alisema ilichukua sehemu kubwa ya maisha yake, pamoja na kazi ngumu.

46 Kisha nikagundua, ninaamini ndivyo ilivyokuwa, kwenye goti la kulia. Sanamu hiyo ilionekana kamilifu, nyororo, na Musa akiwa na kile kibao cha amri mkononi mwake, na ndevu zake ndefu. Na ilikuwa, bila shaka, ni wazo la kiakili la Michelangelo, jinsi ambavyo sura ya Musa ingepaswa kuwa. Labda kamwe hakuwa ameona picha moja, bali, katika mawazo yake, alichora picha ya vile alivyodhania kwamba Musa angalipaswa kuwa.

47 Nayo hadithi inasema, mara alipomaliza ile—ile sanamu, na kuisugua kabisa na kikamilifu, alisimama nyuma kuangalia kazi yake. Na wakati alipovuviwa sana, mpaka ikaonekana sana. . .Kile alichokuwa nacho niani mwake, amekifanya kwa mkono wake. Kilifanana sana nacho, na miaka yote aliyokuwa akikingojea, mpaka akachukuliwa sana na uvuvio, akapiga kwenye goti na kusema kwa sauti kuu, "Nena!" Na kuna kipande kilichomeguka kwenye—kwenye—kwenye mguu, goti la Musa, pale ambapo Michelangelo alipiga kwa nyundo yake, kwa kuwa alikuwa amevuviwa sana.

48 Unaona, kulikuwa na kitu fulani ndani yake, hapo mwanzo, ambapo alichora picha ya kiakili ya vile alivyowazia Musa alipaswa kuonekana. Na wakati alipoona kitu hicho kimeakisiwa mbele yake, kitu kile kile alichokuwa nacho mawazoni mwake, vile alivyowazia Musa anapaswa kuonekana alivyo; na akabeba ono hilo miaka na miaka hiyo yote, alipochukua kipande hicho cha matale, na kubambua kipande hapa na kipande pale, na kukitia alama, maana ilibidi itokee

kikamilifu. Ndipo wakati ilipokamilika mbele zake, alininii—aliona akikiso la yale aliyokuwa nayo niani mwake. Hicho ndicho kilichomvuvia sana, hata akaipiga hiyo sanamu, na kusema kwa sauti kuu, "Nena!" Miaka yake yote ya kazi ngumu ilikuwa imemridhisha. Kazi yake maarufu ya mikono yake ilikuwa imemalizika.

49 Sasa tunaona ya kwamba, na mimi—na mimi nilivuviwa nayo, maana niliwazia ya kwamba, kwa kweli, ile alama kwenye mguu, ndiyo iliyoifanya, kwangu mimi, kuwa kipeo. Kwa sababu, ninii tu, ni kana kwamba tu ni picha nyingine, ama kitu fulani cha Musa, namna fulani ya sura ambayo mtu fulani alikuwa ameiwazia. Lakini, mtu aliyekuwa akifanya kazi hiyo, ilimridhisha sana mpaka akaipiga. Na alama iliyo juu yake iliifanya kipeo kwangu mimi, kwa maana iliakisi kikamilifu kile kilichokuwa niani mwake yale Musa aliyopaswa kuonekana alivyo.

50 Loo, nilisimama pale. Ilinibidi kuzungukazunguka kwa dakika chache kutoka kwenye hiyo picha, kuwazia juu ya—juu ya kile jambo hilo lilichomaanisha kwake, na—na kile lilichomaanisha kwangu mimi wakati huo. Ndipo likanijia mawazoni mwangu, juu ya jambo hili ninalotaka kuwazungumzia habari zake.

51 Hebu sasa na tugeuze mawazo yetu kutoka kwa Michelangelo, tuyaelekeze kwa yule Mchongaji mkuu, Mungu Mwenyenzi, Ambaye, hapo mwanzo, kabla hakujakuwa na siku wala mapambazu ya siku, kabla hakujakuwa na atomi au molekuli. Mungu, katika nia Yake, alimwazia mwanadamu, jinsi ambavyo mtu anapaswa kuonekana alivyo, jinsi anavyopaswa kuwa, na jinsi anavyopaswa kuishi. Naye alitaka mtu huyo awe ni sehemu Yake, "Kwa hiyo akamfanya mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu akamwumba mtu," loo, wakati Mungu, hapo mwanzo, alipofanya kipeo hiki, kitu ambacho kiliakisi mawazo yake.

52 Kumbuka, kuna namna moja tu ya Uzima wa Milele, na ninii yetu . . . hata majina yetu na mawazo yetu yalikuwa pamoja na Mungu kabla hapajakuwa na msingi wa ulimwengu. Kwa sababu sasa tuna Uzima wa Milele. Na ili kuwe hivyo, tunapaswa kuwa sehemu ya Mungu. Kwa hiyo tunapaswa kuwa vivyo hivyo katika mawazo Yake, maana tuna Uzima wa Milele, na tulichaguliwa tangu zamani kwa ajili ya maisha haya. "Na majina yetu yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu," kulingana na Ufunuo. Sasa, kwamba Mungu alikuwa nasi katika mawazo Yake, ndipo tuna Uzima wa Milele, maana basi Yeye alitunena, nasi tukatokea. Na neno ni wazo tu lililodhihirishwa. Mungu alikuwa pamoja nasi, hapo mwanzo, katika mawazo Yake.

53 Sasa, na wakati alipomfanya Adamu, huyo mtu wa kwanza, jinsi alivyokuwa mkamilifu. Alionekana kama Mungu. Mungu,

yule Roho Mtakatifu mkuu, akiatamia juu ya dunia, Naye... ndege wakatokea, labda, na wanyama, vitu mbalimbali, na vikaendelea kutokea katika mfano wa Yeye aliyekuwa akiatamia. Mpaka, hatimaye, kulitokea kiumbe kilichofanana kabisa na Yeye aliyekuwa akiatamia, Mungu. Mungu alikuwa, ama...Mwanadamu alifanywa katika mfano wa Mungu, basi, wakati alipomweka katika bustani hii kuu. Kama vile Michelangelo ameweka kazi yake kuu ya maisha yake, na wachongaji wote mashuhuri; Mungu aliweka kazi ya mikono Yake katika bustani ya Edeni, akamfanyia msaidizi. Ilikuwa ni ri—ri—ridhaa kamilifu jinsi gani kwa Mungu, mpaka hata Yeye akapumzika. Ilikuwa tu ni mapumziko. Kazi Yake ilikuwa imekwisha.

Ndipo hadithi ya kuhuzunisha inakuja, ya adui.

54 Sasa angalia. Jambo hili moja ninataka mlishike, kwamba Mungu alimpa mtu huyu ulinzi, alimpa. Alimlinda ndani ya Neno Lake, kwa maana Yeye aliwaambia yale wangeweza kufanya, yale wasingeweza kufanya.

55 Na huo ndio msingi ule ule tuliowekewa leo, yale tunayoweza kufanya, yale tusiyoweza kufanya. Haidhuru sisi ni wazuri jinsi gani, jinsi gani tunavyoenda kanisani, ama kufanya jambo hili, hatuna budi kuzaliwa mara nyingine. Unaona? Lazima tuzaliwe.

56 Basi Mungu alimwambia Adamu yale ameruhusiwa kufanya na yale asingeweza kufanya. Alimweka nyuma ya Neno Lake.

57 Ndipo adui alipoingia, kwa udanganyifu, na kunyemelea kupitia katika kuta za Neno la Mungu, maana alikuwa amefunguliwa mlango, naye akauharibu ule mfano, kwa dhambi. Hiyo ni moja ya hadithi za kuhuzunisha sana.

58 Ukiwazia, kwamba mtu aliyefanywa katika mfano wa Muumba Wake, na akapewa ukuta asimame nyuma yake, kwamba Neno hilo lisingeweza kamwe kushindwa. Hilo—hilo ndilo tumaini la Mkristo. Ni ngao ya—yake. Ni silaha zake. Ni mwamba wake siku hizi, ni, kukaa nyuma ya Neno; kila mwamini.

59 Sasa, haikupasi kamwe kutoka nyuma ya Hilo. Unapoondoka, wewe, unamfungulia adui mlango, wakati wanaposema, "Loo, vema, unaweza kufanya jambo hili *kidogo*, na jambo lile *kidogo*." Mungu anakutaka ujitenge na kila kitu kinachoitwa dhambi. Ujiweke wakfu kabisa kwa ajili Yake, na kwa ajili Yake tu.

60 Yeye ana kusudi maishani mwako, kila mtu binafsi, ambalo hakuna mtu mwingine usoni mwa dunia anayeweza kupachukua mahali pako. Mungu ana jambo fulani kwa ajili yako. Umefanywa jinsi hiyo. Ulifanywa jinsi hiyo kwa kusudi fulani. Mungu ni mkuu katika kazi Yake. Yeye hata...Mambo tofauti. Sisi ni tofauti, mmoja kwa mwingine.

61 Tunaona katika maisha ya mnyama. Tunaona, katika maisha ya mnyama, kuna mnyama mmoja, Mungu alimfanya mnyama wa kazi, kama farasi, na—naye hana budi kufanya kazi. Na ng'ombe ni sadaka. Na, lakini, si—simba na chui-milia wanazurura mwituni bila kazi yo yote wala cho chote. Alimfanya mnyama mkubwa kama ndovu, kisha akamfanya jamaa mdogo kama panya. Sasa, ni nani aliyeko wa kumwambia Mungu kwamba afanye nini na jinsi ya kulifanya? Anafanya mambo kwa njia Yake mwenyewe.

62 Naye aliifanya milima. Huyafanya majangwa. Huzifanya ba—bahari. Yeye hufanya nchi tambarare. Hufanya aina moja ya mti, mti mgumu, mtende, na—na kadhalika. Yeye hufanya hivyo.

63 Yeye huwafanya wanadamu tofauti. Yeye hutupa sisi, kila mmoja wetu, mahali pa tofauti. Na mtende hauwezi kamwe kuwa mhikori. Mhikori hauwezi kamwe kuwa mtende. Hakuna mtu anayeweza kupachukua mahali pako, wala usijaribu kupachukua mahali pa mtu mwingine ye yote. Kwa sababu, wewe ni mtu binafsi, kwa Mungu, na Mungu ana kusudi fulani kwa ajili yako. Yeye alikufanya hivyo. Unasema, "Kwa nini alifanya jambo hilo?" Yeye ni mweny enzi. Ana sababu ya jambo hilo kuwa hivyo.

Lakini tunaona kwamba sisi sote tumekingwa na Neno.

64 Huko mbinguni, tunaangalia miili ya kimbinguni. Biblia inasema ya kwamba hata nyota moja inatofautiana na nyingine. Kuna sirusi na hizo zingine mbalimbali. Na Mirihi na Jupita, hizo zote mbalimbali, zinatofautiana zenyewe kwa zenyewe. Jua linatofautiana na mwezi, na mwezi unatofautiana na nyota. Na kuna Malaika na Malaika, kama vile, kuna Maserafi na Makerubi wakuu, katika—katika na daraja. Na hata katika ulimwengu mpya ujao, wafalme wa duniani wanaleta heshima zao ndani ya mji huo.

65 Tutakuwa hivyo daima. Kwa sababu, Mungu si Nyumba ya Sears na Roebuck ya Mambo yote ya kulingana. Yeye ni Mungu wa vitu mbalimbali. Yeye humfanya mtu mmoja wa tabia fulani, na mwingine wa tabia nyingine. Lakini tunapaswa kumtumikia katika njia ambayo Mungu alitufanya, na kuwa na furaha, na kukaa nyuma ya Neno Lake. Na hivyo ndivyo Mungu alivyofanya jambo hilo.

66 Lakini wakati tunapoona kwamba adui alipitia kwenye hilo Neno, akafika kwenye kazi ya mkono wa Mungu, akaiharibu. Na hivyo ndivyo hasa anavyofanya sasa. Ananyemelea kwenye hiyo kazi ya mikono, ndivyo adui anavyofanya, akijaribu kutuwekea Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Naye mwanadamu ameninii...Mbona, watu hata hawezi kupatana mmoja kwa mwingine, tutaendaje kuufanya ulimwengu mzima ukubaliane na mwanadamu? Na mara unapofanya jambo hilo...

67 Tunaye mmoja ambaye hatuna budi kudumu katika upatano naye, huyo ni Mungu. "Na hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Naye Neno anabaki kuwa Mungu, na daima atakuwa Mungu, kwa maana Mungu yuko katika Neno. "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu," katika Utu wa Mwana wa Mungu.

68 Sasa tunaona, ya kwamba, baada ya Yeye kuona uharibifu huu mkuu. Ilionekana kama, kama ingalikuwa ni wewe ama mimi, na tumetumia wakati wote na jitihada, tungalikipigilia teke mbali kitu hicho na kuachana nacho. Lakini, si Mungu. Yeye hakuridhika kazi yake iharibike. Huo ni upendo wa Mungu. Si ajabu mhariri alisema:

Kama tungaliijaza bahari kwa wino,
Na kama mbingu zingalifanywa kwa ngozi;
Na kila bua duniani liwe kalamu,
Na kila mtu kazi yake awe ni mwandishi;
Kuandika upendo wa Mungu juu
Kungeikausha bahari;
Ama kama gombo lingaliweza kuenea yote,
Hata likitandazwa kutoka mbingu hata mbingu.

69 Unaona upendo wa Mungu! Baada ya mwanadamu kuanguka na kumfungulia adui mlango makusudi, na akaingia na kumharibu, na kuweka mauti ndani yake, hata hivyo Mungu hakutaka jambo hili lishindwe. Alishuka na kuanza kila kitu upya tena. Alikuwa akitaka kumfanya mtu huyo tena.

70 Yeye alimweka adamu kwenye agano, "Fanya jambo *hili*, wala si *hili*; *hili*, wala si *lile*; usiguse, usishike, usionje."

71 Lakini tunaona, wakati alipoanza tena, Yeye alianza na—na Ibrahimu. Na katika Ibrahimu Yeye alimwanzisha kwenye agano lisilo na masharti. Si "kama utafanya." Nimefanya. Nimelifanya tayari. Nimekubariki, wewe na uzao wako, na kadhalika, baada yako." Lilikuwa ni agano lisilo na masharti. Alianza na Ibrahimu. Ustadi Wake, na sasa pamoja na agano Lake lisilo na masharti. Halafu, tunapoona, Yeye alianza na Ibrahimu na kumpa agano, lisilo na masharti, lenye ahadi.

72 Ndipo akaja kwa wale wazee, tunakuja, katika Agano la Kale, tunaposhuka chini. Hapa alionyesha msingi wa kazi Yake. Sasa tuna Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Yusufu; wale wazee wanne.

73 Sasa, Ibrahimu aliwakilisha kazi ya imani, imani, maana Ibrahimu alikuwa ni imani. Alikuwa na imani kubwa, kwa sababu, "Hakusita katika ahadi ya Mungu, kwa kutokuamini. Wakati, tungesema, "mambo yameenda mrama," na kila kitu kilikuwa kinyume naye, yeye angali alimshikilia Mungu.

74 Halafu tuna Isaka, aliyekuwa ni mwana aliyependwa, ambaye aliwakilisha upendo. Kwa sababu, Ibrahimu akiwa ni mfano wa Mungu, kwa kuwa Isaka alitolewa dhabihu, Mwanzo

22. Tunaona kwamba yeye alibeba kuni akapanda kilima. Na kila kitu kilionyesha picha ya Kristo, kilikuwa ni kivuli Chake. Na ndipo kondoo dume alikuja naye akatolewa badala yake.

Sasa hiyo ilikuwa ni imani, upendo.

75 Na *Yakobo*, ambalo maana yake ni "laghai," na huyo ni mwongo. Nasi tunatambua ya kwamba maisha ya Yakobo kwa kweli yaliwakilisha neema, kwa sababu ilikuwa ni neema ya Mungu, wakati wote, kwa Yakobo.

76 Ndipo akaja Yusufu. Hakuna neno dhidi ya Yusufu. Yeye alikuwa ndiye yule mtu aliyekamilishwa. Nabii wa Mungu aliyetoka miongoni mwa ndugu zake. Naye alionewa kinyongo, bila sababu, na akauzwa. Na katika kila njia, maisha yake yalikuwa ni kivuli cha Yesu Kristo. "Alikuja kwa walio Wake, walio Wake hawakumpokea." Kama vile Yusufu alivyochukiwa na ndugu zake, akatupwa shimoni, akidhaniwa kuwa amekufa; akatolewa, akapandishwa kwenye mkono wa kuume wa Farao. Na wakati alipokiacha kiti cha enzi, walipiga tarumbeta, unajua, kila goti lilipaswa kupigwa, na kwa Yusufu.

77 Tunaona ya kwamba Yesu aliuzwa kwa karibu bei ile ile ambayo Yusufu aliuzwa. Akatolewa shi—shimoni; akapaa Mbinguni; ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Na wakati atakapotoka mahali hapo, "Baragumu italia, na kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri Kwake," ukamilifu.

Hiyo ilikuwa ni imani, upendo, neema, na ukamilifu.

78 Ndipo kazi ya mwili inakuja, ya mchongaji huyu mkuu. Alifanya kazi ya mwili kwa manabii. Manabii walikuwa ndio kazi ya mwili.

79 Ndipo hatimaye kikaja kichwa cha mwili huu mkuu, ambacho kilikuwa ni Kristo Mwenyewe. Manabii wote walikuwa wametabiri habari zake. Kazi yote ya msingi ilikuwa imetabiri habari Zake. Kote kote kutoka katika bustani ya Edeni, kutoka wakati ule ule alipoanza, "Nitaweka uadui kati ya uzao wako na uzao wa nyoka." Nasi tunaona ya kwamba Yeye alianzia pale, kisha akaja kupitia kwa—kwa wazee wetu akaingia kwa manabii, kisha akatokea pale. Mara nyingine tena aliona akisisho Lake mwenyewe, wakati mtu mmoja alipozaliwa duniani, kutoka katika tumbo la uzazi la mwanamke, ambacho kilikuwa ni Kipeo cha Mungu. Ilikuwa ni Mwana wa Mungu, Yesu Kristo. Sababu ya Yeye kuwa hivyo, ni kwa sababu alikuwa ni Neno kikamilifu.

80 "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu."

81 Sasa tunaona kipeo kikamilifu kimeakisiwa katika Yeye. Yeye alikuwa mkamilifu sana, kama Mungu, mpaka akasema, "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, msiniamini. Ingawa

Mimi . . . Hamwezi kuniamini Mimi? Aminini hizo kazi, kwa kuwa zinawashuhudia, Mimi ni Nani." Ninapenda jambo hilo. Unaona? Yeye alisema, "Msiponiamini Mimi . . . "

Wao wakasema, "Wewe ni Mwanadamu, ukijifanya sawa na Mungu."

82 Akasema, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi nizifanyazo. Na kama sizifanyi kazi Zake aliyenipeleka, basi hamna haki ya kuniamini Mimi."

83 Ndivyo impasavyo kila Mkristo, leo, kuwa na ushuhuda ule ule. Kama katika Neno hili la Mungu lililoahidiwa, kama maisha yetu hayafaulu na kutimiza vile Neno lilivyosema hasa, basi hatuna haki ya kujiita wenyewe Wakristo kama hatujazaliwa mara ya pili. Yesu alisema, katika Marko 16, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Unaona? Si "huenda zikafuatana; zinapaswa kufuatana; labda zitafuatana." Sharti zitafuatana. Huyo ndiye Mchongaji aliyetufanya. Hilo ndilo Kanisa lililokatwa. Huo ndio—huo ndio Mwili wa Kristo.

84 Sasa tunaona ya kwamba ilimwakisi kikamilifu. Yule Mchongaji sasa alikuwa amelifanya Neno kuakisi kwenye kile Kipeo tena, kilichoitwa Mwanawe, Mungu, Imanueli. Wazia tu, ya kwamba, mtu ambaye amejidhili sana mpaka Mungu akajitambulisha Mwenyewe mle ndani, katika mwili huo, Naye akawa . . . Yeye na Mungu wakawa mmoja. "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Baba Yangu anaishi ndani Yangu. Mimi daima hufanya lile linalomfurahisha Baba."

85 Vipi kama Mkristo siku hizi angeweza kuwa na ushuhuda kama huo? Ungekuwa ni kipeo papa hapa Yuma, mtaani. Kama wewe ni dobi mwanamke huko nje nyuma beseni la kufulia, ungali utakuwa ni kipeo kwa Mungu, wakati unapoweza kusema, "Daima nafanya kile kinachompendeza Mungu," na ulimwengu mzima unaweza kuona ka—kazi ya Yesu Kristo ikiakisi ndani yako.

86 Inasemwa, wakati mmoja, ile dhahabu ya kale, kabla hawajakuwa na kiyeyusha. Ninii . . . Walikuwa wakichukua dhahabu na kuipiga, yule mpigaji angeipiga, hao wahindi katika siku za mwanzoni wakati Arizona ilipokuwa inaanza. Waliipiga hiyo dhahabu mpaka huyo mpigaji akaona akisisho lake mwenyewe katika dhahabu hiyo. Waliipiga wakatoa vipande vyote vya chuma, mavi yake, takataka, kutoka kwake, mpaka huyo mpigaji aliweza kuona akisisho lake kama kioo, akiipiga kabisa.

87 Sasa, hivyo ndivyo Injili inavyofanya. Watu wengi sana hawataki kugeuzwageuzwa na kupigwa vilivyo. Vema, kile kanisa linachohitaji usiku wa leo ni kupigwa kuzuri kwa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu, kwa ulimwengu na mambo ya ulimwengu. Hicho ndicho Pentekoste inachohitaji usiku wa leo. Hicho ndicho mashirika yetu yanachohitaji usiku wa leo, ni

kugeuzwageuzwa hasa na kupigwapigwa kwa dhahabu kwa mtindo wa kale, mpaka ulimwengu wote umepigwa ukatolewa kutoka kwetu, naye Yesu Kristo amedhihirishwa.

88 Hebu nipate kundi hili la watu hapa usiku wa leo, waliomwamini Kristo kabisa, na maisha yao yamewekwa wakfu kwa Kristo. Ninaweza kufanya zaidi kwa hawa wachache, ama Mungu anaweza kufanya zaidi, hasa, na watu hawa wachache sana hapa, kuliko ungaliweza kufanya na Baraza zima la Makanisa Ulimwenguni, katika Ufalme wa Mungu. Mtu mmoja aliyejisalimisha kabisa mikononi Mwake, huyo tu ndiye Mungu anayehitaji.

89 Lakini, unaona, hatutaki kukaa kimya na kumwacha apige upande *huu*, upande *ule*, agonge atoe kitu *hiki*, agonge atoe *kile*, agonge atoe wazo *hili* nje, na *lile*, na kumwacha Yesu Kristo adhihirishwe ndani yetu. Tunatazama sinema nyingi kupita kiasi. Tuna televisheni nyingi kupita kiasi. Tuna burudani nyingi kupita kiasi za duniani, mpaka kanisa limepoteza ladha yake kwa watu. Ni kwa sababu Roho Mtakatifu anatoka nje, na kitu kingine kinaingia ndani. Hiyo ni kweli, enyi marafiki.

90 Ninasikia shuhuda, wale Wapentekoste wa mtindo wa kale, jinsi walivyokuwa na mikutano ya maombi usiku kucha. Baba zetu na mama zetu, miaka arobaini, hamsini iliyopita, wanaomba usiku kucha. Watu waliwachukia, mtaani. Nasi tunafikiri, siku hizi, kama mtu ye yote hatupigipigi begani, mbona, tuna kasoro fulani. "Ole wenu wakati watu wote watakapowanena mema." Yeye alidharauliwa na kukataliwa na watu, na sisi ni uakilishi Wake. Amina.

91 Kile tunachohitaji siku hizi ni mikutano halisi, ya dhati ya maombi, kufagia kabisa, kote kote kutoka mimbarani hata kwa bawabu, nyumba yote inapaswa kufagiwa, ya Mungu, kupigwa, ipate kuakisi Sura ya Mpigaji, Injili ikihubiriwa katika nguvu za kufufuka kwa Kristo. Hiyo ni kweli.

92 Maskini injili hii ya mkumbo tunayoenda nayo, na kumbembeleza *huyu*, na kumfanya *huyu* shemasi, na *yule* mzee wa kanisa, ama kitu kama hicho, yote ni siasa. Hivi hivyo sivyo hasa ilivyotendeka huko Nikea Rumi? Tunataka kuachana na upuzi huo. Wamethodisti, Wabaptisti, Mpresbiteri, Wapentekoste, na wote, inatupasa tutoke kwenye jambo hilo.

93 Siasa si sehemu ya Kanisa. Roho Mtakatifu anapaswa kulitawala Kanisa, wala si kura za siasa za nani ni nani. "Mungu aliweka kanisani wengine mitume, wengine manabii, na wengine waalimu, na wainjilisti, na wachungaji," si watu waliwapigia kura waweko. Mungu aliwaweka pale, kwa kuitwa na Roho Mtakatifu, mikutano ya maombi, na kuwekea mikono, na kukaa mbele za Mungu.

94 Lakini, siku hizi, tumeifanya dini yetu kupendwa na watu sana kufikia mahali ambapo ni karibu ni kama siasa, yenyewe,

tunayofanya katika madhehebu yetu yote. Tunaninii. . .Mtu mmoja hawezi kumwelekezea kidole huyo mwingine. Sisi sote tuna hatia. Miongoni mwao unakuta wanaume fulani halisi na wanawake halisi. Lakini shida, kile ninachowazia, tunafikia zaidi sana kwenye—kwenye upande wa uchache, watu walio halisi ambao wanataka kuamini na wanaotaka nguvu za Mungu. Kuna wengi mno wanaoletwa kimkumbo, "Vema, *huyu* ni mtu mnyofu. Yeye ni mtu mpole."

95 Tuna makanisa mazuri. Tunajenga makanisa mazuri, na makanisa bora zaidi kuliko tuliyowahi kuwa nayo. Hiyo ni sawa. Hakuna kitu dhidi ya jambo hilo. Ninapenda kuona kanisa likifanikiwa.

96 Lakini, ndugu, afadhali nilione likifanikiwa katika nguvu za Bwana kuliko kufanikiwa katika mambo ya kidunia. Rudini kwenye Injili tena! Rudini kwenye nguvu za Mungu! Rudini pentekoste, ninii. . .kama ile ya kwanza ilivyokuwa. Lakini, unaona, shida yake ni kwamba, hatutaki huko kupigwa.

97 Unaweza kusema jambo fulani kuhusu jambo fulani, na mambo ya uzinzi ambayo kanisa linafanya, ama—ama jambo fulani la kijamii, mara moja wanakukataa, wanaifunga milango. Huwezi kuingia, unaona, kwa sababu wanafanya mkutano nao wanakukataa. Hawakutaki tena. Wanasema, "Una kichaa. Umerukwa na akili." Lakini mradi tu ni BWANA ASEMA HIVI, hilo kwangu mimi halinisumbui kile mtu ye yote anachosema. Inahitajika nguvu za Kristo kumbadilisha mtu. Inachukua nguvu za Kristo kumshikilia mtu.

98 Na kama vile Yesu alivyosema wakati mmoja, "Yatafakarini maua. Na hata hivyo nawaambia ya kwamba Sulemani, katika utukufu wake wote, hakupambwa kama moja." Sulemani, katika utukufu wake wote, alikuwa ni tamasha la fahari. Hapana shaka. Alikuwa ni kazi iliyo kuu kwa dunia, na mtu mkuu mbele za Mungu. Lakini joho la Sulemani halikuwa na uhai ndani yake. Lilikuwa ni kipande cha kitambaa, labda kimetokana na sufu ya mgongoni mwa kondoo. Lakini, ua lilikuwa na uhai.

99 Kile tunachohitaji siku hizi ni Uzima wa Kristo ndani yetu. Huo ndio unaosafisha; si nje, ukosi uliopinduliwa, ama digrii ya saikolojia, ama kitu fulani. Inahitaji nguvu za Kristo aliyefufuka kutufanya kile tunachopaswa kuwa, Mungu hana mpango mwingine wo wote zaidi ya kumwacha Roho Mtakatifu aongoze na kutawala Kanisani.

100 Loo, Mungu, Yeye alikuwa sana sana katika sura ya Mungu, mpaka Yeye na Mungu wakawa Mmoja. "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja." Loo, jamani! Hayo yalikuwa ni maisha ya namna gani, kwa Mungu kuishi ndani Yake hivi, hata kwamba maisha Yake yakawa yamefungwa katika Mungu. Si ajabu kilikuwa ni kipeo!

Shetani alimjia.

101 Kila wakati Mungu alipodhani ya kwamba ana kipeo, Shetani aliingia. Aliingia kwa Musa, naye akazivunja zile amri. Bali alipokuja kwenye Kipeo hiki, hicho kilikuwa ni chaguo la Mungu mwenyewe. Amina. Alikuwa—alikuwa amemchagua tangu zamani. Haikumfaa kitu. Aliishi mwaminifu kwa Mungu, wakati Mungu alipomwangalia na hata akaona alijaribiwa siku arobaini jangwani, kama Musa. Bila shaka, watu hao wote walikuwa ni kivuli Chake. Torati ilivunjwa. Lakini wakati alipokuja, Shetani, yule mjaribu mkubwa, na alijaribu kumjaribu Yeye, aliona kwamba hakukutana na Musa pale. La, bwana. Yeye aligusa voti ya wati elfu tano iliyoziunguza mbawa zake wakati alipomrukia kumshambulia Huyo.

102 "Imeandikwa," Yeye alisema. Unaona? Adamu alianguka chini. Lakini Yesu, Adamu wa pili, kile Kipeo kilichokuwa kimekuja, kwa ajili ya Mkombozi, Yeye alisema, "Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno linalotoka katika kinywa cha Mungu.'" Hapo alikuwa na Kipeo. Naam, bwana. Alisema kitu kingine. Alisema, "Imeandikwa pia. 'Usimjaribu Bwana Mungu wako.' Nenda zako nyuma, Shetani." Hicho hapo Kipeo. Yeye alifanya nini?

103 Sio kusema, "Nitaliambia kanisa langu. Nitawaambia wazee wa kanisa kufanya mambo *fulani*. Askofu atafanya mambo *fulani*."

104 Yeye alisema, "Imeandikwa." Hilo ndilo alilomweka Adamu wake wa kwanza nyuma yake, naye akaanguka, na Shetani akakitia doa. Bali asingeweza kum chafua Huyu, hata angefanya nini. Sana sana, mpaka yeye . . .

105 Mungu alisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa. Msikieni Yeye. Kila kitu, ninampa Yeye kila kitu. Ninyi, msikieni Yeye." Walikuwa ni Mmoja. Walikuwa ni kitu kimoja. Mungu aliishi ndani Yake, akimfanya Yeye kuwa Mungu, Imanueli, duniani. Yeye alikuwa ndiye Mwana-Kondoo mkamilifu, loo, Kipeo kikamilifu cha ukombozi. Ilimpendeza Mungu, basi, kama tu vile Michelangelo, Yeye alivuviwa sana na maisha Yake. Tunaona katika . . .

106 Nina Maandiko yaliyoandikwa hapa chini. Marko 9:7, kama mkitaka kuyasoma. Wakati . . . Ni Mlima wa Kugeuka Sura. Wakati alipokuwa huko juu ya Mlima wa Kugeuka Sura, tunaona ya kwamba alitokea Musa, na akatokea Eliya.

107 Na kisha, muda si muda wajua, mtume Petro alivuviwa sana, hata akasema, "Na tujenge maskani tatu hapa. Tutaunda tu madhehebu matatu kutokana na jambo hili. Tutaunda madhehebu matatu: moja la Musa, moja la Eliya, na moja kwa ajili Yako.

108 Wakati alipokuwa akinena, palitokea sauti kutoka katika lile wingu. Ilisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninafurahia

kuishi ndani Yake, nitampiga kwa ajili yenu. Msikieni Yeye. Yeye atazungumza."

109 "Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu. Alichubuliwa kwa maovu yetu." Yeye alikuwa Mwana-Kondoo, Mwana-Kondoo wa Mungu, Dhabihu kamilifu. Hakujakuwako kamwe na mtu ye yote aliyepata kuishi kama Yeye, na hakujawahi kuishi mtu kama Yeye baada yake. Yeye alikuwa ni Kipeo kikamilifu, alilingana na Neno la Mungu kabisa.

110 Mungu hapo mwanzo alitoa Neno Lake, sehemu kwa ajili ya sehemu *hii* ya wakati, kwa ajili ya sehemu *ile*, kwa ajili ya sehemu *ile*.

111 Hapo ndipo wanadamu wanapodanganywa sana na kutatanishwa siku hizi. Wanajaribu kujenga juu ya jambo fulani lililotukia miaka arobaini, hamsini iliyopita. Tunaninii . . . Hilo, hilo lilitolewa kwa ajili ya wakati huo.

112 Ingelimfaa nini Musa kuja na—na ujumbe wa Henoko? Ingemfaa nini Musa kuja na—na ujumbe wa Nuhu? Ingemfaa nini Yesu kuja na—na ujumbe wa Musa? Unaona? Na ingefaa nini kwa Wesley kuja na Ujumbe wa Luther? Ingelifaa nini Pentekoste kuja na ujumbe wa Wesley? Mnaona ninalomaanisha? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

113 Yote yamepangiwa hapa katika Biblia, na inatubidi kujua wakati na saa, na ni mambo gan i yanayotupasa. Na hapo ndipo tunaposhindwa siku hizi. Tunasoma kila kitu ila Biblia. Hii ndiyo siku tunayopaswa kuishi. Hii ndiyo siku ambayo Mungu ametuweka hapa. Hebu tuangalie katika Neno.

114 Hivyo ndivyo wanavyoshindwa kumwona Yesu; hao Mafarisayo, na Masadukayo, Maherodia. Madhehebu mbalimbali ya siku hiyo yalikuwa yamepanga mambo sana, na kuyapanga kikamilifu sana, hapakuwapo na njia nyingine ya kutokea, walidhani. Lakini wakati Yeye alipokuja, alikuja kabisa . . . Alikuwa tofauti na vile hao wote walivyodhania. Yeye alikuwa maskini Jamaa mdogo, mnyenyekevu aliyezaliwa katika hori, kwa . . . akidhaniwa ni Mwana haramu, na mambo hayo yote namna hiyo.

115 Lakini, hata hivyo, Yeye alikuja vile vile hasa Maandiko yalivyosema Yeye angekuja. Nao walikuwa wamezoea yale Musa aliyokuwa amesema, naye Musa alinena habari Zake. Yeye alisema, "Vema, kama mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi. Musa alinena habari Zangu." Na bado wasingeweza kuona jambo hilo. Walikuwa wamejipinda tu katika mapokeo yao hata wasingeweza kuona hilo. Lakini, unaona, Yeye hakuja kuakisi hayo madhehebu ya siku hiyo. Hakuja kuakisi dini ya kimadhehebu.

116 Yeye alikuja kumwakisi Baba, naye Baba alikuwa ni Neno. Amina. Sasa najisikia wa kidini mno. Alikuja kuakisi Neno la Baba. Mungu alisema Yeye angekuwako, na huyo hapo, kipeo

kikamilifu cha kazi kuu ya mkono wa Mungu. Loo, jamani! Yeye alikuwa ni akisho kamilifu Lake. Aliakisi kila kitu ambacho—ambacho Mungu alikuwa amenena habari zake. Aliakisi yale Adamu aliyokuwa amesema juu Yake. Aliakisi kuhusu yote waliyosema manabii, kuhusu yote waliyosema wazee wetu. Kila kitu alichosema Yeye, alikuwa ni utimilifu wa Neno. Mifano yote ilitimizwa katika Yeye. Naam. Alifanyika Yehova wa Agano Jipya. Alikuwa ni Yehova wa Agano la Kale. "Neno la saa hiyo," lililokuwa katika Nguzo ya moto, "lilidhihirishwa na kukaa kwetu." Yehova wa Agano la Kale akawa Yesu wa Agano Jipya. Yeye alikuwa ni akisho kamilifu la Mungu.

117 Loo, laiti kama Kanisa leo lingaliakisi tu lile Kanisa la kwanza, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka kwenye Siku ya Pentekoste! Laiti Wakristo siku hizi wangaliakisi! Sisi ni kundi la machotara, kulinganisha na vile walivyokuwa.

118 Nilipita, nilipokuwa nikija leo. Nilikuwa nikiangalia hapa chini, karibu na maskini hii Casa Grande, ama baadhi ya makazi haya madogo hapa. Niliona kulikuwako na sha—shamba la pamba, na alfalfa mbalimbali. Ilibidi wawe na vinu vya upepo kule, kuvuta maji, kuliendeleza. Kwa nini? Si mahali pake. Bila shaka si mahali pake. Lakini, angalia maskini mpungate wa kale, kusingenyesha mvua kwa miaka mitano nao ungeishi. Nawe hebu ukose kuumwagilia maji kwa siku chache, na ingekufa. Unaona, si wa asili.

119 Hivyo ndivyo tulivyo. Inatubidi kubembelezwa, na kufanywa watu wakubwa kanisani, na kubembelezwa, na kuitwa *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*.

120 Vema, hao Wakristo wa mwanzoni walikuwa wakali. Hawakujali ni nani aliyewabembeleza. Walimwakisi Yesu Kristo, sana, hata wakasema walijihesabu walio . . . Walikuwa hawana elimu wala maarifa. Hawakwenda kwenye shule ya sekondari ya juu, wala hawakuwa na digrii ya chuoni. "Bali walitambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu." Hicho ndicho wanachohitaji, Wakristo leo, kutambua ya kwamba umekuwa pamoja na Yesu." Kuna kitu fulani ulicho nacho, ambacho ni tofauti. Ninajua hilo si . . . Hilo ni jambo lisilopendwa na watu kusemwa, bali hatutafuti kupendwa na watu. Wakristo hawatafuti jambo lililo rahisi.

121 Dada fulani ajuza kanisani mwangu miaka kadhaa iliyopita, alikuwa akisimama na kuimba wimbo huu:

> Je! yanibidi kuchukuliwa nyumbani Mbinguni
> juu ya kitanda cha maua ya urahisi,
> Wakati wengine walipigana wapate kushinda
> tunzo na wakaabiri bahari zilizojaa damu?
> La. Inanibidi kupigana kama italazimu
> kutawala.

122 Wazia ungefanya nini kama ulikuwa hapa na kila kitu kilikuwa dhidi ya Yesu Kristo, kama ungaliishi katika siku Zake. Unaishi kule, ndugu, dada. Hiyo ni kweli. Yeye angali ni Neno. Angalia jinsi wanavyolikanyaga leo. Angalia jinsi wanavyokazana kulifanya madhehebu, na kuliunganisha, na kila kitu namna hiyo, pamoja na udunia. Jitokeze. Chukua ninii yako—chukua msimamo wako kwa ajili ya Yesu Kristo na Neno Lake. Usiruhusu kitu cho chote kizuie jambo hilo. Kaa moja kwa moja pamoja Nalo.

123 Kama maskini yule dobi wa kale Mchina, alikuwa akija hapa Arizona na California, miaka kadha iliyopita. Asingeweza kuandika neno moja la Kiingereza. Hakukifahamu. Unampelekea nguo zako za kufua. Unajua atakalofanya? Angechukua vipande vichache vya karatasi, hakuna kitu kilichoandikwa juu yake hata kidogo. Yeye angekirarua tu kipande hicho cha karatasi na akupe kipande kimoja. Utakaporudi, kipande hicho cha karatasi kilipaswa kulingana na kipande chake cha karatasi, la sivyo usingepata nguo zako zilizofuliwa. Hilo ni zuri zaidi. Ungeweza kunakili jina, bali hutampumbaza kwa jambo hilo, maana kipande hicho cha karatasi hakina budi kulingana kikamilifu na kipande chake cha karatasi.

124 Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya agano Lake pia. Ujuzi wetu si wa kulinganishwa na kanuni ya imani, mafundisho fulani ya sharti, madhehebu fulani ya kanisa, bali ni wa kulinganisha na Neno la Mungu, Yesu Kristo. Kweli. Tunapomjia Kristo, basi Kristo anatudai. Yeye alimpasua vipande viwili, hapo Kalvari. Sehemu yake Yeye aliitwaa juu, na kuiweka kwenye mkono Wake wa kuume, ambayo ilikuwa ni mwili. Roho, Yeye alikuja, alitumwa kurudi hapa kumfanyia Yeye Bibi-arusi. Na ujuzi uo huo uliokuwa katika Kristo hauna budi kuwa ndani yetu.

125 Yeye alikuwa—Yeye alikuwa mkamilifu sana hata ilimpendeza Mchongaji, na kumvuvia sana mpaka akampiga pale Kalvari. Loo, jamani! Sasa tunamwona kama Maandiko yalivyosema, Kipeo cha Mungu. "Tunamwona amepigwa, akang'otwa, na kuteswa na Mungu." Hicho hapo Kipeo halisi. Kama vile 'Angelo alivyokipiga chake, hilo ndilo lililofanya . . .

126 Kama angalikuwa ameishi maisha mazuri, Yeye angalikuwa tu kama baadhi ya watu ambao wanahubiri injili ya kijamii ya siku hizi, "Yeye alikuwa ni nabii." Alikuwa ni nabii, bali alikuwa ni zaidi ya nabii. Alikuwa ni Mungu. Alikuwa ni Imanueli.

127 Na sasa kilichomfanya hivyo hasa, kwangu mimi, Ki—Kipeo kwangu na kwako, ni kwa sababu Mungu alimpiga. Alimpiga pale Kalvari. Kama hangalipigwa . . . Haidhuru aliwafufua wafu wangapi, jinsi gani alivyohubiri sana, maisha Yake yangekuwa ni makuu jinsi gani, jinsi gani madai Yake yalingekuwa, Yeye alithibitishiwa pale. Alipendezwa sana, Mungu alipendezwa, mpaka Yeye akawa ndiye Mtu wa pekee ambaye alipata

kusimama juu ya uso wa nchi ambaye Mungu angeweza kumpiga kwa ajili ya wengine wote. Yeye aliye mkamilifu alipigwa kwa ajili ya wasio wakamilifu. Uumbaji wote uliokuwa umeanguka, kupitia kwa Adamu, ulikombolewa kwa njia ya Yesu Kristo. Kipeo cha Mungu kimestahimili jaribio. Yeye alifanyaje jambo hilo? Kwa Neno. "Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.'"

128 Loo, rafiki Mkristo, vaa silaha yote ya Mungu. Usibaki nyuma ukiwa na wazo hafifu la kanuni fulani ya imani, au kitu fulani unachosimamia. Vaa silaha yote ya Mungu unapokwenda kupigana na adui, kama vile Bwana wetu alivyofanya. Yeye alionyesha jinsi ambavyo Mkristo aliye dhaifu sana anavyoweza kumshinda Shetani kwa Neno tu. Yeye alikuwa na nguvu, angeweza kumtwanga Shetani kwa mbinu yoyote aliyotaka, bali hakuzitumia. Alichukua tu Neno na kumshinda nalo Shetani. "Imeandikwa. Imeandikwa." Kila mahali, "Imeandikwa." Kwa hiyo akamshinda Shetani kwa Neno la Mungu.

129 Sasa, hicho kilikuwa ni Kipeo kikamilifu na Mungu akakipiga. Ilikuwa ni mfano wa jinsi gani! Ni jambo halisi jinsi gani! Nena kuhusu kipande cha sanaa ya kuchongwa ya—ya Michelangelo kule, kuhusu Musa akipigwa mguuni? Biblia ilisema, "Mtu huyu aliumbuliwa zaidi ya watu wote. Aliumbuliwa sana hivi kwamba hata hakuonekana kama Mwanadamu. Alipigwa. Alijeruhiwa. Alikuwa amejaa damu. Alivuliwa nguo." Yeye...Kila kitu ambacho kingaliweza kufanywa. Alionekana kama lu—lundo kubwa tu la Damu na mifupa, ikitembea pamoja. Hata hakuonekana kama mwanadamu, alipokuwa akiukokota huo kwenda Kalvari. Mungu alimpiga kwa ajili yetu. Huko ndiko kunakomfanya Kipeo kikamilifu.

130 Loo, jinsi ninavyompenda, kujua kwamba alifanya jambo hilo kwa ajili yangu, kujua ya kwamba alifanya jambo hilo kwa ajili yako. Tunawezaje—tungewezaje kulinganisha jambo hilo? Hakuna mtu angaliweza kulilinganisha. Hakuna mtu anayestahili kulingana nalo. Tuko hapa bila tumaini. Tuko bila Mungu. Tuko bila njia yo yote ya ukombozi. Kila mmoja wetu amezaliwa kwa kujuana kimwili, na ilitubidi tu kulipia gharama. Bali Yeye alikuja, Yule mkamilifu, naye alikuwa ni mkamilifu sana na mwenye kupendeza sana hata Mungu akampiga kwa ajili yako na kwa ajili yangu.

131 Sasa, kwa karibu miaka elfu mbili, Mungu amekuwa akijaribu kujikatia Bibi-arusi kipeo, anayeitwa Kanisa. Hiyo ni kweli. Mungu anafanyaje jambo hilo? Yeye hulifanya kwa njia yake isiyobadilika, lile Neno. Mungu habadili njia Yake hata kidogo. Mtu ye yote, unaweza. Unabadilika. Mimi ninabadilika. Wakati unabadilika. Ulimwengu unabadilika. Bali Mungu habadiliki, Yeye ni mkamilifu. Habadiliki. Na jinsi anavyofanya

kitu cho chote mara ya kwanza, Yeye hukifanya kila wakati namna hiyo hiyo.

132 Yeye alimwokoa mwanadamu wakati mmoja kwa sababu alitubu. Hivyo ndivyo atakavyomwokoa mwanadamu tena. Alimponya mtu mmoja kwa sababu alikuwa na imani. Yeye atamponya anayefuata juu ya msingi ule ule. Yeye habadilishi njia Yake kamwe, kwa sababu, unaona, Yeye ni mwenye enzi na ni wa Milele. Yeye hana kikomo, yuko kila mahali, ana nguvu anajua yote. Yeye ni Mungu. Na kwa hiyo haimbidi kumwuliza mtu ye yote apate hekima. Hana haja ya kungojea mpaka ajifunze zaidi. Hahitaji digrii mpya. Yeye ni mkamilifu. Na digrii yo yote, na kitu cho chote anachofanya kwanza, uamuzi wake wa kwanza unadumu vivyo hivyo milele. Hauwezi kubadilishwa. Loo, jinsi nilivyo na furaha!

133 Na wakati alipofanya kipeo Chake cha kwanza, Yeye alimweka nyuma ya Neno. Alipokifanya Kipeo Chake cha pili, Yeye alikuwa ni Neno. Amina. Yeye alikuwa ni Neno; si *nyuma* ya Neno. Lakini, Yeye alikuwa ni Neno. Mungu kamwe habadilishi mpango Wake. Hivyo ndivyo alivyoanza kufanya na kanisa lake la kwanza, Neno.

134 Sasa, Mungu, Neno, hapo mwanzo Yeye alikuwa huru na wengine wote, kila kitu, watu wengine wote. Sasa, simaanishi kusema jambo hili nipate kuwa tofauti. Mungu ni mbaguzi. Je! mnajua jambo hilo? Mnazungumza kuhusu kuunganisha? Mungu ni mbaguzi. Kwa hakika Yeye hubagua. Huwatenganisha watu Wake na ulimwengu. Aliwatenganisha Israeli, taifa Lake. Yeye anajaribu kulitenganisha kanisa Lake na ulimwengu, bali kanisa linataka kuendelea na ulimwengu. Lakini watu Wake wangali wamebaguliwa, wametengwa Kwake. Yeye ni Nani? Neno.

135 Mtu anawezaje kupata na ubatizo wa Roho Mtakatifu, naye Roho Mtakatifu ndiye aliyeliandika Neno, na mtu apate ubatizo wa Roho Mtakatifu na alikane Neno? Roho Mtakatifu ndani yako anawezaje kukana Neno Lake Mwenyewe lililotengwa kwa ajili yako? Siwezi kuelewa na jambo hilo. Hana budi kukubaliana na Neno. Na kama roho yako ndani yako hataitikia kila Neno la ahadi za Mungu kwa "amina," kuna kasoro fulani.

136 Ndugu Fred Sothmann ama mtu fulani hapa usiku wa leo, alinukuu, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Yeye ni Neno. Hilo, ni hakika. Yeye daima ni yeye yule, unaona, na roho yako haina budi kuitikia hilo kwa "amina."

137 "Loo, Yeye, kwa njia moja ndivyo alivyo." Ni kwa kila njia, yeye yule jana, leo, na hata milele.

138 Sasa tunaona ya kwamba Mungu alianza kumfanyia Bi— Bibi-arusi kwa ajili ya Kristo. Kwa hiyo. . . Na Bibi-arusi hana budi kutambulishwa pamoja Naye na katika Yeye, kwa sababu yeye ni sehemu Yake. Sasa, Bibi-arusi ni sehemu Yake. Bibi-arusi ni sehemu Yake. Hilo Neno kwa ajili ya siku hiyo, Bibi-

arusi anakuwa sehemu ya Neno hilo, kwa kuwa ni Kristo. Sasa, mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Inatupasa kuwa katika Kristo. Katika Kristo, inatupasa kuwa wa Kristo, ndani ya Kristo, sehemu ya Kristo.

139 Mwanamke ni nini, wakati anapoolewa na mwanamume, ama mwanamume anapomwoa mwanamke? Mwanamke huyo hana budi kuwa ni sehemu yake. Si wawili tena. Ni mmoja.

140 Na wakati Mungu na Kristo walipofanyika mmoja, walikuwa ni Mmoja. Maana, Mungu alikuwa ni Neno, nalo Neno lilifanyika mwili. Mwili na Neno vikawa kitu Kimoja. Na wakati kanisa linapokuwa Bibi-arusi wa Kristo, Yeye na hizo Injili ni Mmoja.

141 Unawezaje kusema, basi, "Siku za miujiza zimepita"? Unawezaje kusema, basi, "Yeye si yeye yule jana, leo, na hata milele"? Unawezaje kusema, "Mambo hayo ni kwa ajili ya mtume ama mwanafunzi fulani, ama mtu fulani katika siku nyingine," wakati wewe ukiwa ni sehemu Yake?

142 Wakati, Yeye alisema, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe." Vipi kuhusu Ufunuo 22, wakati alipomaliza kuandika Kitabu hicho? Yeye alisema, "Ninashuhudia ya kwamba kama mtu ye yote ataongeza neno moja, ama ataondoa Neno moja kutoka Kwake, ataondolewa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima."

143 Tunawezaje kwenda Mbinguni, basi, tukisema, "Vema, ninaamini jambo hili, bali siamini Lile"? Huna budi kuwa Neno lote, kwa kuwa wewe ni sehemu Yake. Hivyo ndivyo Mungu anavyojaribu kulifanya Kanisa Lake leo, si kwa kanuni ya imani. Nao wanajaribu kutulazimisha kuingia katika jambo lile, jamani. Mnaweza kuona jambo hilo likija. Maandiko ya mkono yako kwenye ukuta. Haitachukua muda mrefu sana mpaka tutakapokuwa Kanisa la ulimwengu. Na kila kanisa litapaswa kuingia moja kwa moja kwenye hilo, vinginevyo litajuta. Vema, je! uko tayari kustahimili jambo hilo? Afadhali usilifanye ati kwa sababu tu unafikiri ni jambo linalofaa.

144 Afadhali uwe na Kristo ndani yako, maana Neno hilo ni la Milele, na Neno hilo ndilo litakalokufufua tena. Wewe unakuwa sehemu ya Neno hilo. Unatambulishwa pamoja na Neno.

Leo hii, wewe unasema, "Mimi ni Mkristo."

145 "Wewe ni wa madhehebu gani?" Vema, hilo halina uhusiano wo wote na Ukristo.

146 Ni sawa kuwa na madhehebu mengi. Sipingi jambo hilo. Lakini, unaona, hivyo, hivyo ndivyo watu walivyo. Watu wengi wanasema eti mimi ninayashambulia madhehebu, na kuyapiga teke. Siyashambulii. La, bwana. Madhehebu, hayo ni sawa. Hilo ni kama tu jambo la maafikiano ya kufanya kazi, ama kitu cho chote kama hicho. Lakini wakati unapong'ang'ana, kwa kuwa

unasema, “Mimi ni Mkristo kwa sababu mimi ni mfuasi wa kanisa *fulani*,” hilo halimaanishi jambo lo lote. Unapaswa kuwa ni wa Kristo, naye Kristo ni Neno. Na mara nyingi madhehebu hayo yako mbali sana na Neno kama Mashariki ilivyo mbali na Magharibi.

147 Wewe huna budi kudumu katika hilo Neno, upate kuwa Bibi-arusi. Kama wewe uko katika Bibi-arusi, wewe uko ndani ya Neno, nalo Neno liko ndani yako. Na lile Neno lililomwakisi Mungu kupitia kwa Kristo, linamwakisi Mungu yeye yule kupitia kwako. Amina. Amina maana yake ni “na iwe hivyo.” Kwa hiyo, kwa hiyo na iwe. Ninaami kwamba hivyo ni Kweli. Unapaswa kujitambulisha pamoja Naye.

148 Sasa, kama nitakuwa Mmarekani halisi na wa kweli, kama nitakuwa mwananchi halisi wa taifa hili, sina budi kutambulishwa nalo. Inanibidi kuwa yote lililowahi kuwa, mazuri au mabaya. Sina budi kuwa yote liliyo, mazuri ama mabaya; yote litakayokuwa, lizuri ama libaya. Inanibidi kujitambulisha na taifa hili, kama nitakuwa Mmarekani. Hiyo ni kweli? Katika utukufu wake ama aibu yake, uhuru ama umaarufu wake, cho chote lilicho, sina budi kuwa mhusika wa sifa zake za kudumu. Sina budi kuungana nalo. Kila kitu lilicho, ndicho nilicho. Kila kitu lilichopata kuwa, ndicho nilichokuwa. Yote litakayopata kuwa, sina budi kuwa mshiriki wake. Hiyo ni kweli.

149 Hebu wazia jambo hilo kwa dakika chache. Basi, napaswa kuwa hivyo, kama Mmarekani. Nitawafahamisha, ili kwamba mwe na hakika kuliona, wakati nikifunga.

150 Ili kuwa Mmarekani, sina budi kutambulishwa na kila kitu lilichowahi kufanya. Basi, nilitua huko Plymouth Rock, pamoja na—pamoja na babu zetu. Mimi nilikuwako kule Plymouth Rock pamoja na wale Wasafiri. Mimi nilikuwako kule pamoja nao. Nilipanda farasi pamoja na Paul Revere, usiku mmoja, kulionya taifa hili juu ya hatari zake. Ilibidi niwe hivyo, kama nilikuwa Mmarekani.

Unasema, “Loo, Ndugu Branham!”

151 Hebu ngoja kidogo. Biblia ilisema, katika Waebrania mlango wa 7, ya kwamba, “Levi aliyepokea zaka, alitoa zaka, kwa kuwa alikuwa katika viuno vya Ibrahimu wakati alipokutana na Melkizedeki, babu wa babu yake, na ilihesabiwa kwake. Wakati kitukuu chake kilipokuwa katika viuno vyake, wakati Ibrahimu alimtolea zaka Melkizedeki, Mungu alimhesabia. Je! alifanya jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hiyo ni kweli.

152 Cho chote kile taifa hili lilicho, ndicho mimi nilicho. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, nilitua kule Playmouth Rock. Nilipanda farasi pamoja na Paul Revere.

153 Nilivuka Bonde la Forge, nilikuwa kwenye ule mto wa barafu pamoja na George Washington. Nilikuwa mmoja wa

hao askari wa Kimarekani ambao hawakuwa na viatu, kwenda kukabiliana na Waingereza. Nilikuwa na miguu yenye baridi asubuhi hiyo wakati nilipofunika miguu yangu. Nilimwona Washington akitoka nyikani, amelowa maji, mpaka kwenye kiuno chake, kutokana na kuomba usiku mzima. Nilikuwapo pale wakati lilipotendeka.

154 Nilisimama pamoja na Stonewall Jackson, wakati upinzani ulipokuwa mkubwa sana. Wakati majeshi ya kaskazini yalipopelekwa kule chini, wao walisema, "Majeshi yote yamerudi nyuma."

Wakasema, "Yuko wapi Jackson?"

155 Wakasema, "Yeye anasimama kama ukuta wa mawe." Mimi nilisimama pamoja naye pale; maskini jamaa mdogo, mwenye macho ya bluu.

156 Wakati mmoja walimwuliza, "Unawezaje kusimama wakati upinzani ni mkuu jinsi hiyo?"

157 Mtu asiye na majivuno kabisa, alipiga buti lake, namna hiyo, akasema, "Sipitishi kamwe maji mdomoni mwangu, kabla sijamshukuru Mwenyezi Mungu." Nilisimama naye katika msimamo wake. Nilisimama pamoja na Stonewall Jackson. Hiyo ni kweli.

158 Nilikuwa kwenye Karamu ya Chai ya Boston. Nilisaidia kutupa baadhi ya hiyo Chai ya Waingereza baharini. Ilibidi niwe hivyo, nipate kuwa Mmarekani. Naam, bwana. Naam, bwana. Nilitia sahihi Azimio la Uhuru, pamoja na Thomas Jefferson. Nilipiga Kengele ya Uhuru, tarehe 4 Julai, 1776.

159 Nimetambulishwa katika aibu ya kimapinduzi, wakati ndugu alipopigana na ndugu, na baba dhidi ya mwana. Sina budu kutambulishwa katika aibu yake, kama vile vile ninavyotambulishwa katika utukufu wake. Hiyo ni kweli kabisa.

160 Nilikuwa kwenye Kisiwa cha Wake wakati askari wote walipopoteza maisha yao. Niliwaona wakiyapoteza. Niliwaona wakati walipokiteka Kisiwa cha Wake. Nilisaidia kuinua bendera huko Guam. Hakika.

161 Yote lilichokuwa, na yote liliyopata kufanya, yote liliyo sasa, ninajivunia kusema mimi ni sehemu yake, kwa maana ninafurahi kuwa Mmarekani. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

162 Kuwa Mkristo, sina budi kuwa vivyo hivyo. Haleluya! Naam, bwana. Kama mimi ni Mkristo, basi nilihubiri Injili na kuwaonya juu ya hukumu zijazo, pamoja na Nuhu. Naam, bwana. Nilikuwa sehemu yake zamani zile, kule ndani. Nilikuwa sehemu ya mpango wa Mungu.

163 Nilikuwa pamoja na Musa kwenye kijiti kilichowaka moto. Nilifukuzwa toka Misri pamoja na Musa. Nilikimbilia jangwani,

na nilikuwa pamoja naye kwenye kijiti kilichowaka moto. Nilisikia sauti Yake. Niliona utukufu Wake. Niliona Nguzo ya Moto huko ya kile kijiti huko nyuma, ikiongea na Musa.

164 Nilikuwa pamoja naye pale Bahari ya Shamu wakati ilipofunguka. Niliona ile Nguzo ya Moto ikitua kwenye Mlima Sinai. Nilikula mana huko jangwani na nikaunywea mwamba uliopigwa. Haleluya! (Sijisikii hamsini na mitano sasa hivi.) Amina. Naam, bwana. Ninakula mana jangwani, pamoja na wana wa Kiebrania huko nyuma jangwani. Nami niliunywea ule mwamba uliopigwa.

165 Nilisimama na Yoshua asubuhi ile wakati alipokuwa akiangalia kuta za Yeriko, naye akamwona Mtu mmoja amesimama. Alichomoa upanga wake akakimbia kukabiliana Naye. Akasema, "Je! Wewe uko upande wetu. Je! uko upande wa adui yetu?"

166 Akasema, "Mimi ni Amiri wa jeshi la Bwana." Nilimwona Yoshua akitupa upanga wake chini. Nilipiga magoti pamoja na Yoshua wakati niliposujudu mbele Zake, Amiri wa Bwana wa jeshi Lake. Niliona kuta za Yeriko zikianguka, tarumbeta ilipopigwa.

167 Nilimwona Yoshua, akasema, "Jua, simama kimya. Na, ewe mwezi, simama juu ya Ajaloni. Usisogee." Niliona jua likisimama kimya, na mwezi haukuacha kutoa mwanga wake. Yote hayo niliyaona yakitendeka.

168 Nilikuwa pamoja na Danieli katika tundu la simba; pamoja na wana wa Kiebrania katika tanuru iliyowaka moto.

169 Nilikuwa pamoja na Eliya, sehemu zile alikokuwa wakati ulimwengu mzima ulipomkataa, na Ahabu na Mayezebeli wao na nywele zao zote zilizokatwa na vitu vya siku hiyo, rangi zao na poda za aina aina, na kila kitu kilicholipata kanisa. Nilisimama pamoja na Eliya, nikatangaza ujumbe ulio msafi usioghoshiwa, juu ya Neno la Mungu. Haleluya! Nilikaa pamoja naye juu ya Mlima Karmeli wakati aliposimama peke yake kule. Nilimwona akiomba moto ushuke kutoka mbinguni.

Nilikuwa pamoja na Daudi wakati alipomwua Goliathi. Utukufu kwa Mungu!

170 Vema, kama Mimi ni Mkristo, ninatambulishwa na hayo yote. Sina budi kuwa ni sehemu yake. Naam, bwana.

Nilitabiri pamoja na Isaya katika siku yake.

171 Nilikuwa pamoja na Yohana pale Yordani wakati alipomwona hua akishuka juu Yake. Nilisimama pamoja na Yohana pale Yordani.

172 Nilimwona akiwaponya wagonjwa; akimfufua Lazaro; akimfufua binti ya Yairo akawa hai tena, baada ya kufa. Niliona hayo."

173 Nimetambulishwa pamoja Naye katika mauti Yake. Nilikufa pamoja Naye hapo alipokufa pale Kalvari, kisha nikafufuka tena kwenye asubuhi ya Pasaka pamoja Naye, katika nguvu za kufufuka Kwake. Mimi ni shahidi wa jambo hilo usiku wa leo. Nilikufa pamoja Naye pale Kalvari, nikafufuka pamoja Naye kwenye Pasaka. Haleluya! Kuwa sehemu Yake, sina budi kutambulishwa pamoja Naye. Nilikuwa nimetambulishwa pamoja Naye katika mauti Yake. Nilitambulishwa pamoja Naye katika mateso Yake. Nilitambulishwa pamoja Naye wakati madhehebu yalipomkataa. Nilitambulishwa pamoja Naye walipomfukuza toka hekaluni, hapo walipojaribu kumtupa, kumwondosha. Nilikuwa pamoja Naye pale. Nilikuwa pamoja Naye katika mauti Yake, nikafufuka pamoja Naye katika ufufuo.

174 Nami nilikuwa pamoja na wale mia na ishirini walipopanda kwenye chumba cha juu. Naam, bwana. Nilishuhudia ule upepo wa nguvu ukienda kasi uliotoka Mbinguni. Nilinena kwa lugha pamoja na waliotiwa mafuta kwenye Siku ya Pentekoste. Haleluya! Nilikuwa kule kwa sababu nimetambulishwa pamoja Naye. Utukufu kwa Mungu! Hiyo ni kweli. Nilihubiri pamoja na Petro, katika Matendo 2. Loo, nilihubiri pamoja naye pale.

175 Nilihubiri pamoja na Paulo kwenye Mlima wa Mirihi, mbele ya wale wakosoaji. Naam, bwana. Ilibidi nihubiri.

176 Nilikuwa pamoja na Yohana kwenye Kisiwa cha Patmo. Niliona ono la Kuja Kwake. Ni mimi. Ni—nilimwona Luther. Nilikuwa pamoja naye wakati alipokuwa katika yale matengenezo.

Nilikuwa pamoja na Wesley.

177 Na sasa niko hapa katika Yuma, Arizona. Haleluya! Nimetambulishwa usiku wa leo, hapa katika Moteli hii ya Stardust, pamoja na kundi la watu wanaoamini jambo lile lile. "Na sasa tumeketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu." Haleluya! Ninakutarajia Kuja Kwake katika utukufu, moja ya siku hizi. Nimetambulishwa pamoja Naye!

> Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
> Alipozikwa, alizichukua dhambi zangu
> akazipeleka mbali sana;
> Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele;
> Siku moja Yeye anakuja, Ee siku ya utukufu!

178 Sasa nimetambulishwa katika ubatizo wa Roho Mtakatifu; si kitu fulani hapa nje mtaani, kitu fulani miaka arobaini iliyopita. Ninao sasa hivi, utukufu na nguvu za Mungu, za msamaha wa dhambi. Ninamwona akiwaponya wagonjwa, akiyafungua macho ya vipofu, ninamwona akitabiri mambo, akiisoma mioyo ya watu. Nimetambulishwa pamoja Naye katika huduma Yake ya siku hii. Utukufu kwa Mungu! Nimetambulishwa pamoja Naye, kwa ajili ya ukombozi katika siku hizi za mwisho.

Ninatumaini kuwa sehemu ya yule Bibi-arusi mkuu anayekuja moja ya siku hizi.

179 Haidhuru ulimwengu ungesema nini, wanaweza kutuita "wenda wazimu, wenye kupagawa, ama Beelzebuli, ama wazushi," cho chote wanachotaka kuwa. Bado mimi ninataka kutambulishwa pamoja na kundi hilo. Ningali niko kule. Ninabaki kule. Nilizaliwa kule. Ninataka kukaa kule. Daima nitakuwa kule, maana Mungu aliniweka kule. Nimetambulishwa. Nililiacha kanisa langu, kuja kujitambulisha mwenyewe na kundi la watakatifu wanaojifingirisha. Mimi ni mmoja wao. Nimetambulishwa pamoja nao.

Wanasema, "Billy, umerukwa na akili."

180 Labda nilirukwa, bali nilipata nia ya Kristo. Nilipata Neno Lake, nilipata Uwepo Wake, nilipata ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele!. . .jali yale mtu ye yote anayowazia juu yake. Hii ni mimi. Mimi ndimi ninayepaswa kufanya utambulisho wangu. Nimetambulishwa pamoja Naye, kwa Neno la Mungu. Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waamini." Nina furaha kutambulishwa na jambo hilo. Naam, bwana.

181 Mnajua, yule maskini mzee stadi wa fidla, wakati mmoja. Mmeisikia hadithi hiyo. Walikuwa na fidla ya kale nao wakaipiga mnada. Walitaka kuiuza, wala hakuna mtu aliyetaka kuinunua. Wakasema, "Ni nani atakayetoa dola moja? Ni nani atakayetoa dola moja na nusu?" Mwishoni, "Ikatangazwa ya kwanza, mara ya pili, dola moja na nusu."

182 Hatimaye maskini mzee mmoja mwenye mvi alitoka kwa wasikilizaji. Mnaijua hadithi hiyo. Akaichukua, akasema, "Hebu niichukue." Akasugua uta wake kwa rosini kidogo, na akaipiga mara chache. Watu wakaanza kulia. Machozi yakaanza kuwatiririka nyusoni mwao, namna hiyo.

183 Na walipofanya hivyo, yule dalali aliichukua tena, akasema, "Ni nani atakayetoa moja," kasema, "dola elfu moja, elfu mbili, elfu tano?"

184 Tofauti yake ilikuwa ni nini? Bwana, yule aliyeijua, yule aliyeitengeneza, alijua jinsi ya kupata kitu fulani toka katika ilichokuwa.

185 Na alimradi tu tunajaribu kuyatoa makanisa yetu kutoka katika kanuni za imani na madhehebu, kamwe hatutaweza. Hebu Mjenzi Mkuu wa binadamu, Ambaye alimfanya mtu kwa mfano Wake, Ambaye anamjengea Bibi-arusi kwa ajili ya jambo lile lile, hebu mguso wa uta wake wa Roho Mtakatifu uliguse Neno hili moyoni mwako wakati fulani, na itakuwa ni mfano wetu ulio bora kabisa. Haidhuru unahudhuria makanisa mangapi makubwa, na ni majina mangapi yaliyo kwenye kitabu, itafaa zaidi kwa Yesu Kristo kuliko makanisa yote, na

madhehebu, na kanuni za imani, na makanisa ya dunia, na madhehebu, katika dunia nzima.

186 Yeye anamfanya Bibi-arusi. Naam, bwana. Yeye anakata vipande sasa, akiukatilia mbali ulimwengu. Loo, kujiunga na kanisa, na kanuni za imani, na madhehebu, na mafundisho ya sharti, lazima yote yakalitiwe mbali yaondolewe kwenye Kanisa; mawazo yao ya kamila, tofauti yao, mafundisho yao na mambo kadha wa kadha. Rudi na umwache Bwana autwae uta. Hebu mruhusu Bwana akuchukue katika mikono Yake, aliguse Neno, aseme, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

187 Utasema, "Amina, Bwana. Nifanye, nifinyange, nifanye, Bwana, kile ninachopaswa kuwa." Ndipo kutakuwako na kitu cha tofauti.

188 Basi, "Kama nikiinuliwa kutoka duniani, Nitawavuta watu wote Kwangu." Naam, bwana.

189 Yeye anakuchonga sasa, anakuchonga ufanane na Neno Lake tu, anakatilia mbali kanuni zote za imani na mafundisho ya sharti na kila kitu, kutoka kwako, akijaribu kurudi kwa Bibi-arusi kwa ajili ya Mwana, kipeo kingine, sehemu ya Neno. Neno!

190 Yesu asingeweza kupachukua mahali hapo. Unakumbuka wakati waliposoma jambo hilo katika kile kitabu? Yeye alisoma tu sehemu ya unabii ule, akaacha yaliyosalia kwa ajili ya siku za mwisho. Tunapaswa kuchukua sehemu hiyo.

191 Kwa hiyo, unaona, Yeye amekata, anataka kulikata Kanisa alitoe, kama tu alivyomkata Mwana, kama alivyomfanyia Bibi-arusi na Bwana arusi. Ili uwe Bibi-arusi Wake, huna budi kuwa sehemu Yake. Si sehemu ya kanuni ya imani, si sehemu ya kanisa, si sehemu ya madhehebu, bali ile sehemu Yake. Ukikatwa kutoka katika mfano mwingine wo wote, haitafaa kitu. Huna budi kukatwa kutoka kwenye Neno. Ulimwengu ukatwe kuondolewa kwako, na kuacha tu Neno pekee liishi ndani yako.

192 Mchongaji mkuu anakutegemea, uwe tayari kusimama na kuchongwa ufanane na matakwa ambayo Neno Lake linayataka. "Katika siku za mwisho nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili. Wana wenu na binti zenu watatabiri." Kristo ndiye Kipeo kilichotambulishwa cha Neno lililofanyika mwili. Unaombwa kujitambulisha wewe mwenyewe katika Yeye, kwa Neno lile lile, upate kuwa kipeo kwa ajili ya Bibi-arusi.

193 Sasa, ndugu zangu, Mungu alikuwa na kipeo wakati huo, kukionyesha kwa dunia, sasa anataka kipeo leo. Je! unakubali? Je! uko tayari, rafiki yangu Mkristo? Je! una hakika kweli kwamba maisha yako yanaakisi sana kwa ajili ya Kristo, haidhuru dunia inasema nini. Wao wanasema, "Umerukwa na akili. Una kichaa. Ulienda na kujiunga na lile kundi la watakatifu wanaojifingirisha." Usiyasikilize hayo.

194 Kama kweli hujaokoka kikwelikweli, na uko katika ule Mwili, na Neno la Mungu limo ndani yako na linajiakisi lenyewe, na Maisha ya Kristo yanaakisi kutoka kwako ndugu, dada, usibahatishe. Sijali wewe ni nani, una ujuzi wa namna gani, hebu ruhusu Neno liakisi kupitia kwako kila siku, kwa sababu Mungu, katika siku hizi za mwisho, anachukua Bibi-arusi kwa ajili ya Mwanawe, Yesu Kristo.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

195 Baba yetu mpenzi wa mbinguni, ni namna iliyokosa ustadi jinsi gani mbele za kundi la watu wenye akili. Elimu yangu inato-. . .haitoshi, Bwana. Ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu aliye mkuu atayazamisha maneno haya ndani ya mioyo ya watu hawa, hivi kwamba wapate kuona yale niliyomaanisha, kama hawakuweza kuelewa katika njia yangu ya kuchanjachanja mambo, Bwana. Lakini, moyoni mwangu, ni—ninaona yale Wewe unayo—unayojaribu kufanya.

196 Ninaamini, Baba, Bibi-arusi hana budi kuwa sehemu ya Bwana Arusi. Hana budi kuwa vile vile kama Bwana Arusi, kwa kuwa Yeye ni sehemu Yake. Hawezi kamwe, kamwe kuwa Bibi-arusi Wake mpaka awe sehemu Yake. Na hiyo ni sehemu ya Neno, leo, ambayo inasema ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

197 Ile punje ya ngano iliyoishi wakati mmoja duniani, na ikaanguka ardhini, iliota katika sura ya punje iliyoingia ardhini. Na, Bwana, kwenye Siku ya Pentekoste Kanisa kubwa lilitokea. Kulitokea punje nyingine ya ngano, ipate kufanywa Bwana Arusi na Bibi-arusi kwa siku ya mwisho.

198 Tuliona, ilianguka, kwa ajili Yake, kwa muda wa miaka elfu moja. Kutoka katika baraza la Nikea, ilikaa ikioza ardhini.

199 Wakosoaji waliandika kile kitabu, *Mungu Asiyeongea*, "Ambaye angewaacha watoto wadogo wafe, na wauawe na simba, na kuchomwa moto. Na wapiganaji wa maonyesho waliwaua Wakristo kwa ajili ya imani yao, na kuwachoma moto kwenye nguzo." Laiti mtu huyo angalikuwa na ufahamu wa kiroho!

200 Hiyo ngano haina budi kuoza ardhini, bali iliota tena, si katika sura iliyoingia nayo ardhini. Iliingia ardhini katika sura ya punje ya ngano, lakini, ilipochipuka, ilikuwa na vijani, kama ngano ndogo inayoota.

201 Hatimaye ilikua ikapitia, kutoka kwa Luther ikaenda kwa Zwingli, na kuendelea mbele, na hatimaye ikafikia kwenye kishada. Ilijigeuza katika siku za Wesley. Ilionekana zaidi kidogo kama ile ngano, na kufanana nayo zaidi kuliko vijani vyake vilivyoonekana. Inarudia tena hali yake.

202 Halafu tunapata kujua, ilitokea, punje, ilifanana sana na ile halisi. Na kama tu ungeweza kushuka na kufungua maganda

yake, utapata kujua. Ile punje ya kwanza ya ngano haina punje ndani yake, hata kidogo. Ni ganda, jani. Bwana, ule uamsho mkuu wa Kipentekoste uliotokea, ilibidi uwe hivyo, Bwana, upate kuilinda Ngano wakati itakapotokea. Kusingekuwa na mahali kwake kwenda.

203 Sasa, Baba, tunajua ya kwamba tunachukulia mambo yote kwa maumbile, kwa sababu Wewe uliyafanya maumbile. Wewe uliikomboa dunia: kwa jinsi ulivyoibatiza, katika siku za Nuhu, baada ya kuhubiri kwake; ulidondosha Damu ya Mwana juu ya dunia, ili kuitakasa kwa ajili yako Mwenyewe; na katika ule wakati mkuu ujao, katika kule kufanyizwa upya, utaiteketeza kwa moto, ili kuteketeza mambo yote ya dunia uyaondolee mbali. Kama unavyomfanyia Mkristo, unamwokoa: unambatiza; unamtakasa; kisha unamfanyizia ulimwengu mpya, na kisha kumdai kama Wako, kwa kumwekea Roho Mtakatifu ndani yake.

204 Tunajua ya kwamba ngano hii inapitia mchakato ule ule. Maumbile yote hutenda kazi vivyo hivyo. Sasa, Bwana, tunapoona ganda sasa likiipisha Punje, likiingia katika mambo ya ulimwengu, Ee Mungu, jalia kwamba punje hizo zitaninii . . . Ga—ganda halina budi kujiondoa, kusudi punje ipate kuingia katika Uwepo wa Mwana. Ninasikia kuja kwa kombaini havesta, Bwana. Haitachukua muda mrefu. Ndipo ile lifti kuu itamchukua Bibi-arusi Wake utukufuni, katika Uwepo wa Mungu.

205 Ninaomba, Baba, ya kwamba utambariki kila mmoja wetu. Hebu na tukumbuke, Bwana, ya kwamba hii ndio nafasi yetu. Huenda tusiwe na moja kesho. Leo ndio nafasi yetu. "Leo, baada ya muda mrefu sana, ukiisikia Sauti Yake, usiufanye mgumu moyo wako." Bwana Mungu, siwajui watu hawa. Kama kuna ye yote hapa, aliyepungukiwa na haya, jalia usiku wa leo ya kwamba watapokea utimilifu wa Mungu, na kujazwa na Roho Mtakatifu. Tujalie, Baba.

206 Sasa huku tumeinamisha vichwa vyetu, mioyo yetu imeinamishwa, pia. Enyi marafiki, samahani jinsi ninavyokatakata ujumbe wangu. Na—naomba ya kwamba Mungu atawaonyesha tu yale niliyomaanisha. Sasa, kama . . . Sitaki mtu ye yote kuangalia. Endeleeni tu kuinamisha vichwa vyenu. Sitaki. Hata uwe nani, kama huna hakika ya kwamba maisha yako . . .

207 Sasa, unaona, kila moja ya hatua hizo, wao walifanya nini? Waliishia katika madhehebu. Nini kingefanyika? Roho aliondoka, kwenda kwa mwingine. Mara Luther alipounda madhehebu; Roho alienda kwa Wesley. Wesley akaunda madhehebu; Roho akaenda kwa Pentekoste moja kwa moja. Pentekoste ikaunda madhehebu; Roho sasa anaenda wapi? Kama tu vile ile Nguzo ya Moto, inaendelea tu kusonga mbele.

208 Na baadhi ya watu wangesema, “Mimi ni Mpentekoste.” Hilo ni jambo zuri. “Mimi ni Mlutheri.” Hiyo ni kweli. Hakuna kitu dhidi ya hilo.

209 Lakini, ewe rafiki, ewe rafiki, Ngano ingali inasonga mbele. Tumekwisha kuwa na mmoja wa ufufuo mkubwa sana. Ume—umedumu muda mrefu zaidi. Historia inaonyesha ya kwamba ufufuo hudumu tu kama miaka mitatu. Huu umedumu miaka kumi na mitano, ama zaidi, kampeni kubwa za uponyaji, bali sasa zimepoa. Angalia! Kila ufufuo husababisha daima madhehebu nyuma yake. Kwa nini huu hukufanya hivyo? Kuna kundi dogo la wandugu walioanza, mahali fulani hapa, liitwalo Mvua ya Vuli, hawakufika po pote; walianguka moja kwa moja kabisa. Kwa nini? Ni wakati wa Ngano, rafiki. Ni Ngano. Kuna huduma duniani ambayo ni kama tu ile iliyoingia ardhini huko nyuma zamani mwanzoni, tukio halisi la Kipentekoste.

210 Makanisa yanaunda madhehebu. Na moja linajaribu kujenga kubwa kuliko lingine, na kupata wafuasi zaidi na kadhalika, madhehebu, polepole. Tunaliona hilo. Eti mimi ni Mpentekoste. Tunaona likiachia. Lakini ni nini? Halina budi kufanya hilo, ili kwamba Mwa—Mwana aweze kuifikia Punje. Kama lisingalikuwa pale pale, kwanza, kama kusingalikuwako na ganda kuifunika, isingalikuwa na mahali pa kwenda. Mungu aliifanya ganda, unaona, kama vile mahindi, kama ngano, kama kitu kingine cho chote kinachotoka katika mbegu zenye miiba. Sasa, unaona, hapajakuwapo na madhehebu yo yote yaliyoanza baada ya haya. Kwa nini? Hakuna wakati mwingine kwa madhehebu. Tuko mwisho.

211 Na kama wewe huko hasa mahali unapopaswa kuwa, nawe ungesema, “Ndugu Branham, kama Mungu atayasikia maombi yako kwa ajili ya wagonjwa, na nimesikia yale Bwana amefanya kwa kuyajibu maombi.” Na umesikia juu ya watu wengine duniani leo, wanaomba. Unasema, “Mimi . . . naomba uniombee, ya kwamba nitapokea tukio hilo, Ndugu Branham? Huenda nisikuone tena.” Huenda nisikuone kamwe. “Bali omba ya kwamba nitakuwako kule. Sijisikii kama tu nitakuwako kule sasa. Lakini ningekutaka wewe uniombee, ya kwamba nitakuwako.”

212 Sasa, kila kichwa kimeinamishwa. Inua mkono wako, tafadhali? Bwana akubariki, akubariki, na wewe. Mungu akubariki. Katika kundi hili la watu, nadhani, mikono hamsini, labda, ama sabini na mitano iliinuliwa.

213 Sasa, Yesu Mpenzi, Wewe ndiye hakimu. Sisi ni wahudumu tu. Ninaomba, Mungu Mpenzi. Na—na kama nimepata neema machoni Pako, jibu ombi langu. Umeona kila mkono ulioinuliwa. Unajua kilichokuwa moyoni mwao. Tunaamini ya kwamba wamechaguliwa kwa ajili ya Uzima. Na Shetani, kama tu katika siku za Adamu, anajaribu kuzuia kipeo hicho kisitokee. Naomba

hilo likomeshwe usiku wa leo. Naomba Damu ya Yesu Kristo lizuie, na jalia watokee kama kipeo kwa Mungu. Tujalie, Baba.

214 Jalia watambulishwe katika Neno la Kristo. Yeye alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili . . ." Jalia wapokee tukio hilo la kuzaliwa mara ya pili. Jalia wapokee ubatizo wa Roho Mtakatifu, kufanyizwa upya kwa mambo yote ya ulimwengu. Hawayataki tena, Bwana. Isafishe hiyo dunia yote iondoke, na uwaweke nje kama kipeo mbele za watu. Tujalie hilo, Bwana, upate kuwa na furaha katika wakati huu wa bustani katika siku hizi za mwisho, upate kuonyesha kipeo Chako cha wanaume hawa na wanawake, wavulana kwa wasichana, walioinua mikono yao. Tujalie, Bwana.

215 Bariki ufufuo huu unaoendelea hapa jijini. Ee Mungu, naomba ya kwamba kila mwanamume na mwanamke, aliye hapa karibu, atatembelea ufufuo huo. Na jalia kila mmoja wao ajazwe na Roho Mtakatifu, na jalia kuwe na ufufuo wa mtindo wa kale utakaoenea mjini humu, mpaka watu kutoka kila mahali watakuja. Tujalie, Bwana. Tupe mambo haya, Baba, kwa kuwa tunayaomba katika Jina la Yesu. Amina.

216 Ninampenda. Ninampenda. Je! unampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnajua, Paulo alisema, "Kama nikiimba, ninaimba katika Roho." Sijui. Mimi niko mbali sana na kuwa mwimbaji. Lakini nashangaa tu, pamoja, kama tusingeweza kuanza kuuimba huo wimbo, *Nampenda*. Waweza kutupa sauti yake, dada? "Kwa kuwa alinipenda kwanza." Mmeusikia? Ni wangapi wanaoujua? Hebu tuone ninii yenu . . . Ni mmoja wa nyimbo zangu za zamani. Ninapenda kuuimba. Vema.

217 Sasa hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu na kufunga macho yetu, na kuimba sasa. *Nampenda*.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

218 Na tuuvumishe. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.] Siku moja pinde za mvua zitajaa hewani. Tarumbeta italia. Waliokufa katika Kristo watakuwa wanafufuka. Loo, jinsi tutakavyolitaka wakati huo!

> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

219 Hapo ndipo alipofanyika Kipeo kwa ajili yetu. [Ndugu Branham anaaza kuvumisha *Nampenda*—Mh.]

220 Kumbukeni tu, vipeo vyote, kabla havijapata kuwekwa kwenye ukumbi wa umaarufu, havina budi kupita katika ukumbi wao wa wakosoaji, kwanza. Wakosoaji wanapaswa kuona kama wanaweza kukikosoa. Lakini wakati

kitakapostahimili wakosoaji, ndipo kinapelekwa kwenye ukumbi wa sifa. Mwana wa Mungu alipitia kwa wakosoaji wa kila shirika, madhehebu, mpaka hata Pilato akasema, “Sioni kosa lake.” Yuda alisema, “Nimeisaliti Damu isiyo na hatia.”

221 Ndipo Mungu alipomfufua, naye ananing’inia katika ule ukumbi mkuu wa umaarufu leo, kwenye mkono wa kuume wa Mungu, akituombea. Hivi hutaki kujiunga Naye kule? Hivi hutaki kuwa sehemu ya jambo hilo? Unaweza kuwa. Umealikwa kuwa. Wakati tukiimba wimbo huu, kwa nini usizungumze mambo yako Naye sasa.

> . . . alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

222 Wakati tukiuimba tena, ninakutaka upeane mikono na mtu fulani upande wa pili wa meza kutoka kwako sasa? Useme, “Mungu akubariki, ewe rafiki Mkristo. Mungu akubariki. Niombee.” Kila mmoja wenu afanye jambo hilo sasa, tunapouimba huu tena.

> Nampenda . . .

Niombeeni. Niombeeni.

> . . . mpenda
> Kwani ali- . . .

223 Naam, peaneni mikono, useme, “Niombeeni.” Nyote niombeeni. Ninataka kuwa kule, mno mno.

> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

224 Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu na kufunga macho yetu, na kuinua mikono yetu na kumwimbia huo sasa.

> Na- . . . Ee Mungu, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

Angalia Kipeo chako kikining’inia pale.

225 Mchongaji mkuu, Mungu mkuu aliyemfanya mwanadamu, na kumfinyanga na kumfanya katika sura Yako wewe mwenyewe, Ninakuomba, Bwana, ya kwamba utatuchukua usiku wa leo. Jalia huu uwe usiku wa kumbukumbu, wa kukumbukwa hasa kwetu, hata, usiku wa leo, Bwana, usiku wa leo, papa hapa katika Moteli hii ya Stardust, naomba uwafinyange watu katika sura ya wana wa Mungu. Tujalie, Bwana. Mchongaji mkuu, Wewe Ndiwe tu unayeweza kufanya jambo hilo. Chukua Neno Lako, Bwana, lifinyange moja kwa moja ndani ya mioyo yetu sote, tupate kuwa vipeo Vyako katika siku za mwisho, na kuitwa Bibi-arusi wa Kristo. Watu wengine waweze kuona ya kwamba kuna ukweli kama huo na furaha kama hiyo katika kumwishia Yeye.

226 Bwana, siku hii, ambayo hata makanisa yetu, wanapoteza uaminifu wao. Hawaninii. . .Inaonekana si waaminifu, kila kitu kimeenda Hollywood. Bwana, ni jambo gani limetukia? Wamefuata ku—kumetameta badala ya mng'ao. Tunajua ulimwengu humetameta kwa ulimwengu. Lakini Injili inang'aa kwa upendo na kwa Kristo. Jalia, Bwana, ya kwamba tutaondokana na kimeto cha ulimwengu, na kuingia katika mng'ao wa Kristo.

227 Hao ni Wako, Bwana. Uliwanunua. Wewe! Waliinua mkono wao, usiku wa leo, walitaka kuwa hayo. Sasa, Baba, mimi. . .Kama ningaliweza, ningaliwafanya hivyo, bali siwezi. Lakini ninakutumainia Wewe. Wewe ulisema, "Yeye anijiaye Mimi sitamtupa nje kamwe. Yeye alisikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni," si ajifanyaye anaamini sasa, Bwana, bali kuamini, "amepita toka mautini kuingia Uzimani." Tujalie, Baba. Hao ni Wako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

228 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye si ni wa ajabu? ["Amina."]

229 Tupe sauti ile ndogo, ama kordi pale, dada, Wa Ajabu, Wa Ajabu.

Mnapenda kuimba? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Je! Ninachukua muda mrefu sana? [Viongozi wa wafanyabiashara wanasema, "La."]

230 Ninapenda kuabudu. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Ujumbe mdogo unaokata kama huu, mimi sininii. . .Mwajua, nachukia kukatakata. Lakini, wewe, huna budi kupigilia msumari, na kuufanya ushike. Mnajua ninalomaanisha? Naam. Huna budi kuupigilia sawasawa sasa. Na unaona?

231 Je! mnaupenda huo wimbo? "Wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu mimi." Mnaujua huo?

Wa ajabu, wa ajabu, Yesu yu kwangu,
Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
Huniokoa, hunilinda kutoka katika dhambi na aibu zote,
Wa ajabu ni Mkombozi wangu, Jina Lake lisifiwe!

Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, sasa nimepatikana, niko huru na hukumu,
Yesu hutoa uhuru na wokovu mkamilifu;
Huniokoa, hunilinda na dhambi na aibu zote,
Wa ajabu ni Mwokozi wangu, Jina Lake lisifiwe!

Kila mtu!

Wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu mimi,
Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
Huniokoa, hunilinda kutoka kwa dhambi na aibu zote,
Wa ajabu ni Mwokozi wangu, Jina Lake lisifiwe!

232 Sasa hebu na tuseme, "Mungu asifiwe!" [Kusanyiko linasema, "Bwana asifiwe!"—Mh.] Bwana asifiwe! Hivi hamjisikii mmesuguliwa? ["Amina."] Mnajisikia vizuri? Mwabuduni Bwana. Yeye ni wa ajabu sana.

233 Mungu awabariki hadi tutakapokutana tena. Nitamwachia ndugu huyu sasa ibada, kiongozi wa ushirika.

*KIPEO CHA MUNGU KILICHOTAMBULISHWA* SWA64-1205
(The Identified Masterpiece Of God)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 5 Desemba, 1964, kwa ajili ya dhifa ya Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Moteli ya Stardust huko Yuma, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2010 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org